JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

# TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2021

**Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015**

**Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2021**

**Imetayarishwa na;**
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,**
**S.L.P 80327,**
**8 Barabara ya Kivukoni,**
**11486 Dar es Salaam**
**Barua pepe : cg@dcea.go.tz**
**Tovuti : www.dcea.go.tz**
**Instagram : @dceatanzania**
**Twitter : @dceatanzania**
**Facebook : @dceatanzania**
**YouTube: DCEATV**
**Simu ya Bure 119**

**ISBN:978-9912-9896-2-7**

**Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015**

## YALIYOMO

YALIYOMO ....i
ORODHA YA MAJEDWALI ....iii
ORODHA YA VIELELEZO ....iv
MAELEZO YA WAZIRI ....v
DIBAJI ....vii
FAHARASA ....viii
**SURA YA KWANZA ....1**
TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI....1
1.1 Utangulizi ....1
1.2 Bangi ....1
1.3 Dawa za kulevya jamii ya Afyuni ....2
1.4 Cocain ....2
1.5 Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya ....3
1.6 Dawa Mpya za Kulevya ....4
1.7 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (ATS) ....5
1.8 UVIKO 19 na Dawa za Kulevya ....5
**SURA YA PILI ....7**
MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEYA NCHINI ....7
2.1 Utangulizi ....7
2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction) ....7
2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction) ....7
2.4 Kupunguza Madhara ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction) ....7
2.5 Kuimarisha Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ....8
**SURA YA TATU ....9**
KUPUNGUZA UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA ....9
3.1 Utangulizi ....9
3.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya ....9
3.3 Udhibiti wa Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya ....20
3.4 Maboresho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 ....23
3.5 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya ....23
3.6 Kesi za Dawa za Kulevya ....25
**SURA YA NNE ....26**
KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA ....26
4.1 Utangulizi ....26
4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya ....26

4.3 Madhara ya Dawa za Kulevya ....................................................................28
4.4 Jitihada Zilizofanyika Katika Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya ....30
**SURA YA TANO ....................................................................................................35**
KUPUNGUZA MADHARA YANAYOSABABISHWA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA ............................................................................................................35
5.1 Utangulizi ...................................................................................................35
5.2 Huduma ya Tiba Saidizi kwa Waraibu kwa Kutumia Dawa (MAT) ...........35
5.3 Nyumba za Uptaji Nafuu (Sober Houses) ..................................................38
5.4 Tiba ya Uraibu wa Dawa za Kulevya katika Vitengo vya Afya ya Akili Nchini ..........................................................................................................41
5.5 Faida ya Huduma za Upunguzaji Madhara kwa Waraibu ....................42
**SURA YA SITA .......................................................................................................44**
USHIRIKIANO WA KIMATAIFA, KIKANDA NA KITAIFA KATIKA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA TANZANIA ..................................................................44
6.1 Utangulizi ....................................................................................................44
6.2 Ushirikiano wa Kikanda ...............................................................................44
6.3 Ushirikiano wa Kimataifa ............................................................................44
6.4 Ushirikiano na Taasisi Nyingine za Kimataifa ..................................45
**SURA YA SABA .......................................................................................................47**
CHANGAMOTO NA HATUA ZA BAADAYE .................................................47
7.1 Utangulizi ..................................................................................................47
7.2 Changamoto ..............................................................................................47
7.3 Mikakati .....................................................................................................47

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 ....................10

Jedwali Na. 2: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 ....................12

Jedwali Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 ....................13

Jedwali Na. 4: Idadi ya Wtuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 ....................15

Jedwali Na. 5: Mwenendo wa Uingizaji wa Kemikali Bashirifu Nchini Kuanzia Mwaka 2018 hadi 2021 ....................17

Jedwali Na. 6: Kemikali Bashirifu zilizozuiliwa kuingia Nchini Mwaka 2017 Hadi 2021....18

Jedwali Na. 7: Orodha ya Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya zilizoingizwa Nchini Mwaka 2021 ....................20

Jedwali Na. 8: Kesi zilizofikishwa Mahakamani Mwaka 2021 ....................24

Jedwali Na. 9: Asasi zilizotoa Elimu ya Dawa za Kulevya Mwaka 2021 ....................32

Jedwali Na. 10: Asasi Zilizowezeshwa na Mamlaka Mwaka 2021 ....................33

Jedwali Na. 11: Idadi ya Waraibu waliopewa Rufaa kutoka Asasi za Kiraia kwenda Vituo vya MAT, Januari hadi Desemba , 2021....................35

Jedwali Na. 12: Waraibu waliopata Huduma ya MAT Mwaka 2011 hadi Desemba, 2021 .....36

Jedwali Na. 13: Waraibu waliopata Huduma Katika Nyumba za Upataji Nafuu kwa Mwaka 2021 ....................37

Jwdwali Na. 14: Idadi ya Waraibu Waliopata Tiba kwenye Vitengo vya Afya ya Akili Nchini kwa Mwaka 2021 ....................40

# ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 .......... 11

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 .......... 11

Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa Waliokamatwa kwa Kujihusisha na Bangi na Mirungi Nchini Kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 .......... 12

Kielelezo Na. 4: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 .......... 14

Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Kiasi cha Heroin na Cocain kilichokamatwa kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 .......... 14

Kielelezo Na. 6: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine Waliokamatwa Nchini Kati ya Mwaka 2012 hadi 2021 .......... 15

Kielelezo Na. 7: Kiasi cha Kemikali Bashirifu Kilichozuiliwa kuingizwa Nchini Mwaka 2017 hadi 2021 .......... 19

# MAELEZO YA WAZIRI

Serikali imeendelea kupambana na tatizo la uzalishaji, matumizi na biashara ya dawa za kulevya Nchini. Kama ilivyokuwa katika kipindi kilichopita uzalishaji, matumizi, biashara ya dawa za kulevya na changamoto za janga la UVIKO 19 yameendelea kuwa tatizo duniani na kuathiri uchumi, jamii na masuala ya ulinzi na usalama.

Kwa upande wa dawa za kulevya za mashambani za bangi na mirungi zimeendelea kuwa tatizo Nchini. Katika mwaka 2021, jumla ya tani **22.74** za bangi zilikamatwa, zikiwa ni ongezeko la asilimia **72** ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2020 na ikijumuisha jumla ya watuhumiwa **9,484.** Mirungi iliyokamatwa katika kipindi hicho ilifikia tani **10.93** zikihusisha watuhumiwa **1,395.**

Kwa upande wa dawa za kulevya zinazozalishwa viwandani, mwaka 2021 jumla ya **tani 1.13** ya heroin ilikamatwa nchini ikiwa ni kiasi kikubwa kuwahi kukamatwa tangu nchi yetu ipate uhuru. Kiasi hicho ni mara tatu ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2020. Aidha, watuhumiwa walikamatwa wakihusishwa na dawa hiyo. Kwa upande wa cocaine, kiasi cha gramu **811.30** zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa **100.**

Kwa mara ya kwanza katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini, shehena kubwa ya jumla ya kilo **430.77** ya dawa za kulevya ya kutengenezwa na kemikali bashirifu aina ya methamphetamine ilikamatwa mwaka 2021, ikihusisha watuhumiwa tisa wote wakiwa wanaume. Katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali inaendelea kufuatilia mwenendo wa uingizwaji na matumizi ya methamphetamine pamoja na kemikali bashirifu ambazo hutumika kutengeneza dawa hizo.

Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya nchini limeendelea kuwepo ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2021, waraibu wa dawa mbalimbali za kulevya wapatao **905,902** walijitokeza kupata tiba. Serikali imejidhatiti kupambana na tatizo la uraibu wa dawa za kulevya ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 huduma za tiba ya uraibu zilikuwa zikipatikana kwenye vituo 11 vya MAT na vituo vidogo (Satellite clinics) vinne na kufanya idadi ya vituo vinavyotoa huduma hiyo kufikia **15,** Nyumba **44** za Upataji Nafuu na Vitengo vya Afya ya Akili katika mikoa mbalimbali.

Nachukua nafasi hii kuwapongeza wadau wote kwa ushirikiano uliowezesha udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika mwaka 2021 pamoja na kuhamasisha jamii kukabiliana na tatizo hili ambalo ni hatari kwa mustakabali wa nchi yetu.

Napenda kuwahimiza wananchi wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika kupambana na tatizo la dawa za kulevya kwa manufaa yetu sote, ikiwemo kutumia simu ya bure namba **119.**

Mhe. George B. Simbachawene (Mb)
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)**


## DIBAJI

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya huandaliwa kila mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015, ambacho kinaielekeza Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuandaa na kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni. Lengo la taarifa ya hali ya dawa za kulevya ni kuwawezesha wananchi kufahamu hali halisi ya tatizo la dawa za kulevya, jitihada zilizofanywa na Serikali kudhibiti tatizo hilo, changamoto zilizopo na mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo Nchini.

Taarifa hii inabainisha hali ya tatizo la dawa za kulevya duniani pamoja na udhibiti. Aidha, inaelezea utekelezaji wa majukumu kupitia mikakati mikuu minne. Mikakati hiyo ni kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya, kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya Nchini.

Vilevile, mafanikio yaliyofikiwa na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka yameainishwa katika taarifa hii. Aidha, mapendekezo na mipango ya baadaye ya kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya imeorodheshwa.

Kwa kuwa tatizo la dawa za kulevya ni mtambuka, taarifa hii inajumuisha shughuli mbalimbali zilizofanywa na wadau wa udhibiti wa dawa za kulevya wa ndani na nje ya nchi. Napenda niwashukuru wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine ikiwemo waliowasilisha taarifa zao ambazo zimesaidia kufanikisha uandaaji wa taarifa hii.



Gerald Musabila Kusaya
**KAMISHNA JENERALI**
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA**
**KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

## FAHARASA

| | |
|---|---|
| **ATS** | Amphetamine Type Stimulants |
| **AU** | African Union |
| **CDC** | U.S Centers for Disease Control and Prevention |
| **CND** | Commission on Narcotic Drugs |
| **DPP** | Director of Public Prosecutions |
| **EU-ACT** | European Union Action against Drugs and Organized Crime |
| **GCLA** | Government Chemist Laboratory Authority |
| **GF** | Global Fund |
| **INCB** | International Narcotics Control Board |
| **IRDO** | Integrated Rural Development Organization |
| **MAT** | Medication Assisted Treatment |
| **NPS** | National Prosecution Services |
| **SETA** | Serve the Tanzania |
| **TAA** | Tanzania Airports Authority |
| **TMDA** | Tanzania Medicines and Medical Devices Authority |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **UNDP** | United Nations Development Programme |
| **UNODC** | United Nations Office on Drugs and Crime |
| **UVIKO 19** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona 2019 |
| **VVU** | Virusi vya UKIMWI |

# SURA YA KWANZA

# TATIZO LA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

## 1.1 UTANGULIZI

Sura hii inaelezea mwenendo wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya duniani kama ilivyoripotiwa katika Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2021. Kama ilivyokuwa katika kipindi kilichopita uzalishaji, matumizi na biashara ya dawa za kulevya yameendelea kuwa tatizo duniani na kuathiri uchumi, jamii na masuala ya ulinzi na usalama. Katika kipindi hiki ambacho kiliambatana na janga la UVIKO 19 soko la dawa za kulevya liliyumba kwa muda. Hata hivyo, biashara hiyo iliibuka kwa kasi kwa kuimarisha na kuboresha mbinu zilizotumika awali zikiwemo njia za nchi kavu na majini, kiasi kikubwa cha dawa kinachosafirishwa kwa mkupuo, masoko ya mtandaoni, vifurushi kwa njia ya posta, matumizi ya ndege za mizigo na binafsi. Katika kipindi hicho dawa za kulevya zilizotumika zaidi ni bangi, dawa za kulevya jamii ya afyuni, cocaine, dawa tiba zenye asili ya kulevya, dawa mpya za kulevya (New Psychoactive Substances - NPS) na dawa za kulevya jamii ya amphetamine (ATS). Hali ya mwenendo wa dawa hizo umeainishwa hapa chini;-

## 1.2 Bangi

Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2021 ilionesha kuwa matumizi na mauzo ya bangi na bidhaa zake katika tovuti za siri (dark web) yaliongezeka mara nne (4) zaidi kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2017. Aidha, idadi ya watumiaji wa dawa hiyo inakadiriwa kufikia milioni 200 hadi kufikia mwaka 2019 ambayo ni asilimia 4 ya watu wote duniani. Ongezeko la utumiaji wa dawa hii ni asilimia 18 katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Taarifa hii ilisisitiza kuwa dawa ya kulevya aina ya bangi ina kiwango kikubwa cha kilevi ingawa watumiaji wake wanatumia bila kujali madhara yake. Hata hivyo, taarifa ilieleza kuwa matumizi ya bangi yanatarajiwa kuongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya watu duniani na kuruhusiwa kwa kilimo na matumizi ya dawa hii katika baadhi ya maeneo duniani.  Kwa mwaka 2021 watumiaji wengi walikuwa Amerika ya Kaskazini kwa asilimia 14.5 na matumizi kidogo yalikuwa Barani Asia kwa asilimia 2.

Hata hivyo, ukamataji wa bangi Duniani umepungua kwa asilimia 35 hii ilichangiwa na baadhi ya maeneo ya Amerika ya Kaskazini kuruhusu matumizi ya dawa hiyo na kusababisha kushamiri kwa biashara hiyo.

**1.3 Dawa za kulevya jamii ya Afyuni**

Dawa hizi zinatengenezwa kutokana na mmea wa afyuni (opium poppy) kwa kuchakatwa na kemikali bashirifu ili kuzalisha heroin na morphine (opiates) na zipo katika kundi la vipumbaza (depressants). Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2021 inaonesha kuwa Kilimo cha mimea jamii ya afyuni kiliongezeka mwaka 2020 hadi kufikia hekta 295,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia 24 ikilinganishwa na mwaka 2019. Hali hii ilichangiwa na kushamiri kwa kilimo cha mimea hiyo nchini Afghanistan ambayo iliongeza uzalishaji duniani kwa asilimia 85 katika mwaka 2020. Halikadhalika, eneo lililolimwa mimea hiyo liliongezeka kwa asilimia 37 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Katika Taarifa hiyo ilikadiriwa kuwa, watumiaji wa dawa za kulevya jamii ya afyuni walifikia milioni 62 ambao ni sawa na asilimia 1.2 ya idadi ya watu wote duniani. Idadi hiyo ya watumiaji inakadiriwa kuongezeka mara mbili zaidi katika muongo mmoja uliopita. Matumizi makubwa ya afyuni yalikuwa Amerika ya Kaskazini kwa asilimia 3.6 na matumizi madogo zaidi yalikuwa barani Ulaya kwa asilimia 0.8.

Kwa mwaka 2019, usafirishaji wa heroin uliripotiwa katika nchi 99 duniani, idadi ambayo ni kubwa ikilinganishwa na usafirishaji wa morphine. Aidha, Ukamataji wa kiasi kikubwa cha heroin ulifanyika barani Ulaya ikiwa ni asilimia 27 ya kiwango chote kilichokamatwa duniani. Vilevile, katika Taarifa hiyo inaonesha kuwa, kiasi cha tani 228 za dawa tiba zenye asili ya afyuni zilikamatwa mwaka 2014 na 2019 ikiwa ni kiwango cha juu kabisa kuwahi kufikiwa.

Ilikadiriwa kuwa katika nchi ya Marekani watu wapatao 50,000 walipoteza maisha kutokana na kuzidisha kiwango cha matumizi ya dawa za afyuni, fentanyl na jamii zake, vifo hivyo ni zaidi ya mara mbili ya vilivyotokea mwaka 2010.

### 1.4 Cocaine

Kutokana na Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2021 kulikuwa na ongezeko la uzalishaji na matumizi ya cocaine ambapo takribani watu milioni 20 walitumia dawa hiyo kiasi ambacho ni sawa na asilimia 0.4 ya idadi ya watu wote duniani kwa mwaka 2019. Dawa hiyo ilitumika zaidi Oceania kwa asilimia 2.7 na ilitumiwa kwa kiwango cha chini Barani Asia kwa asilimia 0.07. Uzalishaji wa dawa hiyo kati ya mwaka 2014 na 2019 uliongezeka maradufu na kufikia makadirio ya tani 1,784 kiasi hiki ni kikubwa kuwahi kutokea. Pia, kiasi kilichokamatwa kiliongezeka maradufu katika kipindi hicho ambapo mwaka 2019 kiasi kikubwa cha dawa hii takribani asilimia 83 kilikamatwa Amerika. Kilimo haramu cha mimea ya coca ambacho kilishamiri mwaka 2018 na kupungua kwa mara ya kwanza kwa asilimia 5 mwaka 2019.

Njia ya usafirishaji wa cocaine kati ya Amerika ya Kusini na Ulaya ambayo ni ya pili kwa ukubwa duniani ilikuwa na mabadiliko ikilinganishwa na kipindi kilichopita ambapo ilionesha kuongezeka kwa magenge ya kihalifu na kutotumia madalali na badala yake waliagiza moja kwa moja kutoka maeneo ya uzalishaji.

### 1.5 Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa tiba zenye asili ya kulevya ni dawa zinazotumika kutibu maradhi mbalimbali lakini zinaweza kuleta uraibu iwapo zitatumika bila kufuata ushauri wa daktari. Kutokana na hatari hiyo dawa hizi zinatolewa kwa usimamizi maalumu. Mfano wa dawa hizo ni Pethidine, Morphine, Tramadol, Fentanyl, Ketamine, Benzodiazepine na Codeine.

Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2021 ilionesha kuwa, kiasi cha Fentanyl na dawa zinazofanana nayo zilizokamatwa duniani kwa mwaka 2019 kilipanda kwa kasi zaidi ya asilimia 60 ikilinganishwa na mwaka 2018. Kwa ujumla kiasi hiki kimepanda mara 20 tangu mwaka 2015 na kiasi kikubwa kilikamatwa Amerika ya Kaskazini. Vilevile, kati ya mwaka 2015 hadi 2019 kiasi kikubwa cha Tramadol kilichokamatwa kilitoka katika nchi za Afrika Magharibi na Kati ambayo ni asilimia 86 ya jumla ya dawa hiyo iliyokamatwa duniani. Aidha, kiasi kikubwa cha Codeine kilikamatwa katika mfumo wa dawa za kikohozi zilizochepushwa Barani Asia.

Mwenendo wa ukamataji wa dawa tiba za jamii ya afyuni unaakisi uwepo wa masoko haramu katika maeneo mbalimbali duniani. Hali ya uzalishaji wa Tramadol ni mbaya zaidi katika nchi za Afrika Kaskazini, Magharibi na Kati. Hata hivyo, masoko haramu ya Tramadol yanapata dawa hiyo kutoka kwa wazalishaji haramu hali inayochochewa zaidi na uwepo wa mahitaji yasiyo ya tiba.

### 1.6 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substances - NPS)

NPS ni dawa zinazotengenezwa kwa kuiga kemikali zilizopo kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa ili kuficha uhalisia wa dawa hizo na kukwepa mkono wa sheria. Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2021 inaeleza kuwa katika miaka ya hivi karibuni, idadi ya NPS duniani zimeendelea kuwa katika kiasi kilekile ambacho ni zaidi ya aina 500 (541 mwaka 2019).

Idadi ya NPS zenye madhara ya afyuni zinazohusiana na fentanyl imekuwa ikiongezeka zaidi ya muongo uliopita na kuendelea kukua zaidi mwaka 2018 na 2019, ingawa ongezeko hilo lilikuwa kwa kasi ndogo ukilinganisha na awali. Kiasi cha NPS kilichokamatwa kimeshuka ikiwa ni pamoja na NPS za jamii ya bangi ingawa Barani Afrika kiasi cha NPS kilichokamatwa kiliongezeka kutoka kilo moja (1) mwaka 2015 hadi kufikia kilo 828 mwaka 2019, halikadhalika Amerika ya Kati na Kusini kilo 60 hadi kufikia kilo 320 katika kipindi hicho.

Matumizi ya NPS katika nchi za Amerika ya Kaskazini yamepungua ingawa yamekuwa yakiendelea zaidi kwa baadhi ya watu wa makundi maalumu (marginalized groups). Matumizi ya NPS yanaonekana kukua kwa kasi au kushamiri kwa nchi za uchumi wa chini na wa kati.

Kwa upande wa udhibiti wa NPS taarifa inaeleza kuwa vyombo vya kupambana na dawa za kulevya vya kitaifa na kimataifa vimefanikiwa kudhibiti kusambaa kwa NPS hasa kwa nchi zenye uchumi wa juu kwa kutumia sheria mbalimbali kukabiliana na tatizo hilo. Biashara ya NPS iliendelea kukua kwenye nchi zenye mifumo dhaifu ya udhibiti, mathalani uwezo mdogo wa kufanya uchunguzi, mapungufu kwenye vyombo vya usimamizi wa sheria na uhaba wa wataalamu wa afya wa kutambua aina za NPS na matumizi yake. Kuongezeka kwa udhibiti katika soko la dawa za kulevya kunasababisha ugumu wa upatikanaji wa dawa hizo hivyo wahalifu kubuni mbinu ya kutumia kemikali zisizodhibitiwa (Pre-precursors and designer precursors) kutengenezea dawa za kulevya.

### 1.7 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (ATS)

Dawa hizi ni kundi la dawa za kulevya linalohusisha aina mbalimbali ya dawa zikiwemo amphetamine, methamphetamine na ecstasy. Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2021 inaonesha kuwa, takribani watu milioni 27 walitumia ATS mwaka 2019 ambao ni sawa na asilimia 0.5 ya watu wote duniani. Kiwango kikubwa cha matumizi kiliripotiwa Amerika ya Kaskazini kwa asilimia 2.3 na kiwango kidogo Barani Afrika kwa asilimia 0.4. Takribani watu milioni 20 walitumia ecstasy mwaka 2020. Matumizi ya dawa hizi kwa njia ya kujidunga yameendelea kusababisha maambukizi ya HIV katika maeneo mbalimbali duniani.

Kati ya mwaka 2015 na 2019 zaidi ya asilimia 95 ya maabara haramu za ATS zilizogunduliwa zilikuwa zinatengeneza methamphetamine na katika kipindi hicho asilimia 72 ya ATS zilizokamatwa zilikuwa ni methamphetamine. Kati ya mwaka 2015 na 2019 karibu asilimia 85 ya maabara za amphetamine zilizoharibiwa duniani kote zilikuwa Barani Ulaya. Katika kipindi hicho, kiasi kikubwa cha methamphetamine kilikamatwa Amerika ya Kaskazini kwa asilimia 49 na asilimia 43 Mashariki na Kusini Mashariki mwa Asia. Aidha, kiasi kikubwa cha amphetamine kilikamatwa Mashariki ya Kati na Kusini Magharibi mwa Asia kwa asilimia 49, Ulaya asilimia 26 wakati ecstasy nyingi ilikamatwa Barani Ulaya kwa asilimia 43 na Amerika ya Kaskazini kwa asilimia 21.

Ukamataji wa kemikali bashirifu zinazodhibitiwa kimataifa zinazotumika kutengeneza methamphetamine umepungua sana katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, kwa sababu watengenezaji wanaendelea kubadili kemikali wanazotumia ili kukwepa kukamatwa. Ukamataji wa ecstasy na amphetamine uliongezeka mara mbili kati ya mwaka 2015 na 2019. Kiwango cha ATS kilichokamatwa kilipanda kwa asilimia 64 kati ya mwaka 2018 na 2019 ongezeko ambalo ni mara sita katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, wakati ongezeko la methamphetamine lilikuwa ni mara kumi katika kipindi hicho.

### 1.8 UVIKO 19 na Dawa za Kulevya

Kuibuka kwa janga la UVIKO 19 kulileta mabadiliko katika mbinu za biashara na mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Katika kipindi hiki soko la upatikanaji wa dawa za kulevya liliyumba kwa muda mfupi na kuibuka tena kwa kasi, ambapo mbinu mbalimbali zilitumika ikiwemo ongezeko la usafirishaji wa kiasi kikubwa

cha dawa kwa mkupuo kupitia njia za nchi kavu na majini, matumizi ya ndege za mizigo na binafsi, masoko ya mtandaoni na kutuma vifurushi kwa njia ya posta.

Katika kipindi hiki matumizi ya bangi na dawa za usingizi nje ya mfumo wa tiba yaliongezeka duniani. Aidha, biashara ya dawa za kulevya na huduma za matibabu kwa waraibu zilizokuwa zinafanyika ana kwa ana zilifanyika kwa njia ya teknolojia ya mtandao, simu na mifumo ya posta. Nchi nyingi zilianzisha huduma ya matibabu kwa simu ili kutekeleza masharti ya kujikinga na UVIKO 19 ikiwemo kubaki nyumbani. Hali hii iliwawezesha watoa huduma za afya kutoa huduma za unasihi kwa kutumia simu. Huduma za matibabu zilirahisisishwa ambapo methadone ilitolewa kwa kutumia mashine maalumu (vending machines) na sindano za kujidungia zilisafirishwa kwa njia ya posta.

# SURA YA PILI

## MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

### 2.1 Utangulizi

Katika kuelezea jitihada zilizofanyika katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya nchini tumejikita katika utekelezaji wa mikakati mikuu minne. Mikakati hiyo ni kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya, kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa. Hivyo, sura hii itaelezea kwa ufupi vipengele vya kila mkakati na sura zinazofuata zitachambua jitihada zilizofanyika kwenye mikakati hiyo.

### 2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction)

Utekelezaji wa mkakati huu ambao hudhibiti uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya Nchini umezingatia masuala yafuatayo; Ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa kuhusu biashara ya dawa za kulevya; Ukamataji wa wafanyabiashara na dawa za kulevya; Udhibiti wa uzalishaji wa dawa za kulevya (Kilimo na Uzalishaji); Udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na kuratibu uteketezaji wa dawa za kulevya.

### 2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction)

Lengo la Mkakati huu ni kutoa elimu ambayo ni nyenzo muhimu ya kuifanya jamii kujitambua na kujiepusha na matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya. Mkakati huu unatekelezwa kwa kutoa na kuratibu uelimishaji juu ya tatizo la dawa za kulevya katika jamii; kuandaa Miongozo ya uelimishaji, kuwaandaa na kuwawezesha watoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya.

### 2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction)

Mkakati huu unalenga katika kutoa huduma za tiba na ushauri kwa waraibu wa dawa za kulevya. Lengo ni kuhakikisha waraibu na jamii iliyoathirika na matumizi ya dawa hizo inapata tiba, hivyo kupunguza madhara ya kiafya, kijamii na kiuchumi. Ifahamike kwamba uraibu wa dawa za kulevya ni tatizo la kiafya na huathiri watumiaji na jamii kwa ujumla, hivyo tiba ni muhimu ili kuwakinga watumiaji na

jamii husika. Maeneo ya msingi ya mkakati huo ni Kuratibu matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya; Kuandaa miongozo ya matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya; na Kufanya usimamizi shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za tiba na unasihi kwa waraibu wa dawa za kulevya.

### 2.5 Kuimarisha Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka linalohusisha mitandao ya kihalifu iliyopo nchi mbalimbali duniani. Mapambano dhidi ya tatizo hili yanahitaji ushirikiano na nguvu za pamoja kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kutekeleza mkakati huu maeneo ya msingi yafuatayo yamezingatiwa; Kutekeleza mikataba na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya; Kuhudhuria mikutano ya kisera na kisayansi kuhusu udhibiti wa dawa hizo; Kubadilishana taarifa na uzoefu baina ya mataifa mbalimbali kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya pamoja na Kushirikisha wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika mapambano hayo.

# SURA YA TATU

# KUPUNGUZA UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA

## 3.1 UTANGULIZI

Sura hii imeelezea jitihada zilizofanyika katika kudhibiti uzalishaji na usambazaji (biashara) wa dawa za kulevya Nchini katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021.

## 3.2 KUDHIBITI UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA

Katika kipindi cha mwaka 2021, Tanzania imeendelea kukabiliwa na tatizo la dawa za kulevya ambazo ni bangi, mirungi, heroin, cocaine, methamphetamine na dawa tiba aina ya morphine. Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, imeendelea kukabiliana na biashara na uzalishaji wa dawa haramu za kulevya nchini. Jitihada zilizofanyika ni pamoja na kufanya operesheni mbalimbali za ukamataji, uteketezaji, maboresho ya sheria, kufuatilia uendeshaji wa mashauri ya dawa za kulevya na kutoa ushahidi mahakamani. Pia, Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka zingine za udhibiti imefanya kaguzi ili kuzuia uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Vile vile, Mamlaka iliweza kubaini mitandao ya kihalifu ya ndani na nje ya nchi inayojihusiha na usafirishaji wa dawa za kulevya.

### 3.2.1 Operesheni na Ukamataji Dawa za Kulevya

Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama imefanya Operesheni mbalimbali za kukamata wafanyabiashara wa Dawa za Kulevya katika kipindi cha Mwaka **2021** na imebainika kuwa wafanyabiashara wa Dawa za Kulevya wameongeza soko jipya la dawa mpya za kulevya aina ya methamphetamine na dawa tiba aina ya morphine**.**

Matokeo ya operesheni za ukamataji katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021 yameainisha watuhumiwa, aina na kiasi cha dawa za kulevya zilizokamatwa kama ifuatavyo:

#### 3.2.1.1 Bangi

Katika mwaka 2021 biashara ya bangi iliendelea kufanyika ambapo kiasi cha tani **22.74** za dawa hiyo zilikamatwa, kiasi hicho ni kikubwa ikilinganishwa na tani **13.23** zilizokamatwa mwaka 2020 kiasi ambacho ni ongezeko la asilimia **72** la ukamataji

wa dawa hiyo. Pia, takwimu za ukamataji zinaonesha kuwa idadi ya watuhumiwa waliokamatwa wakijihusisha na biashara ya bangi mwaka 2021 ilikuwa **9,484 (**kati yao wanaume **8,726** na wanawake **758**) ikilinganishwa na watuhumiwa wa mwaka 2020 ambalo ni ongezeko la asilimia **25.** Ongezeko la kiasi cha dawa na idadi ya watuhumiwa waliokamatwa imetokana na juhudi za Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama na jamii kwa ujumla katika kupiga vita biashara haramu ya dawa za kulevya **(*Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1&2).***


#### 3.2.1.2 Mirungi

Mirungi ni dawa za kulevya za mashambani ambazo pia zimeendelea kuwa tatizo kwa mwaka 2021. Katika kipindi hiki jumla ya tani **10.93** za dawa hii zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa **1,395** (wanaume **1,212** na wanawake **183)** waliojihusisha na biashara hiyo. Watuhumiwa wameongezeka kwa asilimia **20** wakati kiasi cha dawa kilichokamatwa kimepungua kwa asilimia nane **(8)** ikilinganishwa na mwaka 2020 **(*Rejea Jedwali Na.1 na Kielelezo Na.1&2).***


**Jedwali Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**

| Mwaka | Bangi (Tani) | Mirungi (Tani) |
|---|---|---|
| 2012 | 48.70 | 6.22 |
| 2013 | 85.80 | 12.82 |
| 2014 | 81.30 | 15.74 |
| 2015 | 22.01 | 16.60 |
| 2016 | 68.23 | 21.64 |
| 2017 | 52.19 | 67.81 |
| 2018 | 24.30 | 8.96 |
| 2019 | 21.51 | 9.07 |
| 2020 | 13.23 | 11.80 |
| 2021 | 22.74 | 10.93 |

**Kielelezo Na. 1: Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**




**Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**





Takwimu zinaonesha kiasi cha bangi kilichokamatwa kiliendelea kupungua kuanzia mwaka 2017 mpaka 2020 na kupanda mwaka 2021, hii ni kutokana jitihada za pamoja kati ya vyombo vya ulinzi na usalama katika udhibiti wa dawa hiyo. Hali kadhalika, kiasi cha mirungi kiliendelea kupungua kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2021 hii ni kutokana na juhudi kubwa za uteketezaji wa mashamba ya mirungi na kubainika kwa mtandao wa usafirishaji wa dawa hizo.

**Jedwali Na. 2: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi waliokamatwa kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**

| Mwaka | Idadi ya Watuhumiwa – Bangi | Idadi ya Watuhumiwa – Mirungi |
|---|---|---|
| 2012 | 5,548 | 847 |
| 2013 | 1,547 | 581 |
| 2014 | 11,918 | 1,650 |
| 2015 | 13,275 | 1,780 |
| 2016 | 17,889 | 2,397 |
| 2017 | 11,528 | 1,797 |
| 2018 | 9,744 | 1,185 |
| 2019 | 8,865 | 1,170 |
| 2020 | 7,601 | 1,156 |
| 2021 | 9,484 | 1,395 |

***Kielelezo Na. 3:* Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa Waliokamatwa kwa Kujihusisha na Bangi na Mirungi Nchini Kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**




*Kielelezo Namba 3* kinaonesha idadi ya watuhumiwa wa bangi na mirungi kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 imeendelea kupungua ikilinganishwa na miaka iliyopita hii ni kutokana na juhudi kubwa zinazofanyika katika udhibiti wa dawa hizo.

### 3.2.1.3 Heroin

Mwaka 2021 jumla ya **tani 1.13** (kilo **1,124.52)** za dawa ya kulevya aina ya heroin zilikamatwa nchini. Ukamataji wa dawa hizo ni ongezeko la asilimia **222**

ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo kilo **349.81** zilikamatwa. Vilevile, ukamataji huu ni mkubwa kuwahi kutokea katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini. (***Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.4)***.

Kwa mwaka 2021 watuhumiwa waliokamatwa wakihusishwa na biashara ya heroin walikuwa **588 (**wanaume **516** na wanawake **72)** idadi ambayo ni kubwa kwa asilimia **37** ikilinganishwa na idadi ya watuhumiwa wa mwaka 2020. (***Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.4&5)***.


### 3.2.1.4 Cocaine

Katika mwaka 2021 operesheni zilizofanyika maeneo mbalimbali nchini zilifanikisha kukamatwa kwa kiasi cha gramu **811.3** za cocaine pamoja na watuhumiwa **100 (**wanaume **95** na wanawake **5**). Dawa hii inaonesha kuendelea kutopatikana kwa wingi hapa nchini. (***Rejea Jedwali Na.3 na Kielelezo Na.4&5)***.


**Jedwali Na. 3: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**

| Mwaka | Heroin (Kg) | Cocaine (Kg) |
|---|---|---|
| **2012** | 260 | 151 |
| **2013** | 36 | 4 |
| **2014** | 400 | 45 |
| **2015** | 64.75 | 17.79 |
| **2016** | 42.26 | 18.52 |
| **2017** | 185.56 | 4.14 |
| **2018** | 16.94 | 7.67 |
| **2019** | 55.35 | 10.34 |
| **2020** | 349.81 | 4.52 |
| **2021** | 1,124.52 | 0.811 |

**Kielelezo Na. 4: Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**




**Kielelezo Na. 5: Mwenendo wa Kiasi cha Heroin na Cocaine kilichokamatwa kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**





Takwimu zinaonesha kuwa, kiasi cha heroin kilichokamatwa kuanzia mwaka 2018 kiliongezeka na mwaka 2021 kiasi hicho kiliongezeka mara tatu zaidi ikilinganishwa na mwaka 2020. Hali hii ilitokana na juhudi za vyombo vya ulinzi na usalama na

ushirikiano wa kimataifa katika kuwabaini na kuwakamata wafanyabiashara wakubwa ambao mara nyingi hukutwa na kiasi kikubwa cha dawa hizo.

**Jedwali Na. 4: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa Nchini kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**

| Mwaka | Watuhumiwa - Heroin | Watuhumiwa - Cocaine |
|---|---|---|
| 2012 | 400 | 138 |
| 2013 | 75 | 20 |
| 2014 | 584 | 351 |
| 2015 | 474 | 281 |
| 2016 | 716 | 263 |
| 2017 | 1,005 | 243 |
| 2018 | 463 | 148 |
| 2019 | 318 | 31 |
| 2020 | 428 | 80 |
| 2021 | 588 | 100 |

**Kielelezo Na. 6: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa kati ya Mwaka 2012 hadi 2021**




*Kielelezo Na. 6* kinaonesha kuwa kuanzia mwaka 2018 watuhumiwa wa heroin na cocaine waliendelea kupungua hadi mwaka 2019 na kuanza kupanda kuanzia mwaka mwaka 2020 hadi 2021. Hali hii inatokana na kuongezeka kwa ushirikiano kati ya vyombo vya dola na jamii uliosaidia kupatikana kwa taarifa zilizowezesha kubaini mitandao ya wafanyabiashara wakubwa wa dawa hizo.

### 3.2.1.5 Methamphetamine

Methamphetamine ni dawa ya kulevya inayozalishwa kwa kutumia kemikali bashirifu kwenye viwanda au maabara haramu. Kwa mara ya kwanza, mwaka 2021 kiasi cha kilo **430.77** za methamphetamine kilikamatwa nchini kikihusisha watuhumiwa tisa (9) wote wakiwa wanaume. Katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya, haijawahi kukamatwa au kubainika kwa mraibu wa dawa hiyo. Serikali inaendelea kufuatilia mwenendo wa uingizwaji na matumizi ya dawa hii nchini.



*Kilo 859. 36 za dawa za kulevya zilizokamatwa ndani ya jahazi katika eneo la Kilwa Masoko mkoani Lindi zikiwahusisha raia saba (7) kutokea nchini Iran*

### 3.2.2 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu (Precursor Chemicals)

Kemikali bashirifu ni kemikali halali zinazotumika katika sekta mbalimbali za uzalishaji ikiwemo kutengeneza bidhaa za aina tofauti zikiwemo dawa tiba. Udhibiti

na usimamizi wa Kemikali hizi unafanywa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali chini ya Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani namba 3 ya Mwaka 2003 - *Industrial and Consumer Chemicals (Management and Control) Act No. 3 of 2003.* Vilevile, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 5 ya Mwaka 2015 inadhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu ili zisitumike kutengeneza dawa za kulevya. Mfano, mwaka 2021 kwa mara ya kwanza nchi yetu imekamata shehena kubwa ya kilo 430.77 ya dawa za kulevya aina ya methamphetamine ambazo hutengenezwa kwa kutumia kemikali bashirifu pekee.

Katika kipindi cha mwaka 2021, kiasi cha **tani 3,656 na lita za ujazo 855,807** za kemikali hizo ziliingizwa nchini kwa mujibu wa sheria ya usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani namba 3 ya mwaka 2003. Kemikali hizi zinahitaji ufuatiliaji wa karibu na ukaguzi unaoambatana na utoaji elimu ili kuhakikisha kwamba zinatumika katika matumizi halali yaliyokusudiwa na hivyo kudhibiti uwezekano wa kuchepushwa na wahalifu ili kutumika kutengeneza dawa za kulevya. Udhibiti huu huzuia ongezeko la dawa za kulevya nchini endapo kemikali hizo zinapochepushwa. Kemikali bashirifu zilizoingizwa nchini kuanzia mwaka 2018 hadi 2021 zimeainishwa katika jedwali lifuatalo; -

**Jedwali Na. 5: Mwenendo wa Uingizaji wa Kemikali Bashirifu Nchini kuanzia mwaka 2018 hadi 2021**

| Mwaka | Idadi ya Kampuni | Kiasi cha Kemikali | |
|---|---|---|---|
| | | Tani | Lita |
| 2017 | 167 | 116,257.00 | 13,016,466.00 |
| 2018 | 184 | 1,534,064.00 | 11,247,555.00 |
| 2019 | 160 | 249,768.00 | 6,304,971.00 |
| 2020 | 87 | 96,062.44 | 4,256,161.00 |
| 2021 | 57 | 3,655.97 | 855,807.00 |

*(Chanzo: Taarifa za mwaka za Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali)*

Takwimu zinaonesha kwamba, kiasi cha kemikali kinachoingia nchini kinapungua mwaka hadi mwaka hali inayotokana na kupungua kwa uhitaji wake na Udhibiti unaofanywa dhidi ya kemikali hizo.

### 3.2.2.1 Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Kemikali Bashirifu

Katika kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu elimu juu ya udhibiti na matumizi sahihi ya kemikali hizo hutolewa, sambamba na kufanya kaguzi mbalimbali kwa wanaojihusisha nazo. Jumla ya kampuni **35** zinazojihusisha na biashara ya kemikali bashirifu zilikaguliwa mwaka 2021 katika mikoa ya Mtwara,

Dar es salaam, Mwanza, Mara, Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga, Geita, Tanga, Morogoro, Mtwara, Ruvuma, Songwe, Rukwa, Katavi na Tabora.

Ukaguzi na ufuatiliaji pia ulifanyika kwenye kampuni nane (8) zinazojihusisha na usafirishaji wa vifurushi katika viwanja vya ndege na Shirika la Posta. Vile vile, zoezi hili lilifanyika katika vituo vya forodha vya mipaka 17 ya Namanga, Tarakea, Holili, Manyovu, Kasumulu, Tunduma, Horohoro, Mtambaswala, Nakawale, Kabwe, Karema, Mutukula, Kabanga, Rusumo, Mabamba, Sirari na Kasanga.

Kupitia kaguzi na ufuatiliaji uliofanyika, ilibainika kuwepo kwa udhaifu katika kutunza kumbukumbu za matumizi ya kemikali bashirifu jambo ambalo linaweka mianya ya kusababisha uchepushwaji wa kemikali hizo. Hivyo, elimu juu ya utunzaji sahihi wa kumbukumbu za kemikali hizo ilitolewa.

### 3.2.2.2 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu kwa Njia ya Mfumo wa Kimataifa wa Kielektroniki wa Upashanaji Habari - *Pre-Export Notification (*PEN) *system*


Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya hufuatilia taarifa mbalimbali za usafirishaji haramu wa kemikali bashirifu kwenye mfumo huu unaoratibiwa na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (INCB).

Kwa mwaka 2021 Mamlaka ilifanikiwa kuzuia kuingizwa nchini kiasi cha tani **120.3** na lita **35** za kemikali bashirifu kwa kutokukidhi vigezo vya sheria ya kemikali na dawa za kulevya. Kemikali hizo ni Acetone, Potassium permanganate, Toluene na Acetic acid.

**Jedwali Na. 6: Kemikali Bashirifu zilizozuiliwa kuingia Nchini Mwaka 2017 hadi 2021**

| Mwaka | Kiasi (Tani) |
|---|---|
| 2017 | 250.1 |
| 2018 | 23.1 |
| 2019 | 43.6 |
| 2020 | 57.6 |
| 2021 | 120.3 |

**Kielelezo Na. 7: Kiasi cha Kemikali Bashirifu kilichozuiliwa kuingizwa Nchini Mwaka 2017 hadi 2021**




### 3.3 Udhibiti wa Dawa Tiba zenye asili ya Kulevya

Dawa tiba zenye asili ya kulevya ni dawa halali zenye asili ya kulevya zinazotumika kwa ajili ya matibabu ya binadamu na wanyama. Dawa hizi hutolewa kwa maelekezo maalumu ya daktari/wataalamu wa afya kwa lengo la kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi holela. Udhibiti na usimamizi unafanywa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) chini ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba [Sura 219]. Mfano wa dawa hizi ni Pethidine, Fentanyl, Morphine, Tramadol, Ketamine, Benzodiazepines (Diazepam, Xanax, Lorazepam), Codeine na Phenobarbitone.

Dawa hizi zisipodhibitiwa huweza kutumika kama dawa za kulevya kwa watu wa rika mbalimbali wakiwemo waraibu wa dawa za kulevya pale wanapokosa dawa za kulevya. Katika Kudhibiti uchepushwaji wa dawa hizo Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2015 inaharamisha matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya nje ya mfumo halali wa matibabu.

### 3.3.1 Uingizwaji nchini wa dawa tiba zenye asili ya kulevya

Dawa hizi huingizwa nchini kisheria kama zilivyo dawa zingine za matibabu kutokana na mahitaji yake katika kutoa huduma za kiafya. Kuanzia Januari hadi Desemba, 2021 vibali 84 vya kuingiza dawa hizo Nchini vilitolewa kwa kampuni 23. Dawa zilizoingizwa katika kipindi hicho ni kama zilivyoainishwa kwenye jedwali lifuatalo;-

**Jedwali Na. 7: Orodha ya Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya zilizoingizwa Nchini mwaka 2021**

| Jina la Kiambata Hai (Active Ingredient) | Kiasi Kilichoingizwa (Kg) | Nchi Zilikotoka |
|---|---|---|
| Pethidine | 0.79 | India |
| Morphine sulphate | 0.72 | India |
| Methadone | 130 | India |
| Fentanyl | 4.02 | India, Kenya |
| Diazepam | 45.36 | India, Ufaransa na Kenya |
| Lorazepam | 1.58 | Cyprus |
| Phenobarbitone | 470.48 | India, Ufaransa na Kenya |
| Midazolam | 8.73 | India, Ufaransa |
| Buprenorphine | 0.15 | India |
| Bromazepam | 0.66 | Ugiriki |
| Clonazepam | 0.18 | Uswisi |
| Ketamine | 16.51 | India, Ufaransa |
| Ephedrine | 42.58 | India, Ufaransa na Kenya |

Dawa hizo zilisambazwa katika vituo (Hospitali) 290 vilivyosajiliwa kutumia dawa hizo katika tiba hapa nchini na hivyo kuhitaji ukaguzi na ufuatiliaji wa karibu ili kuthibiti uchepushwaji na kutumika kama dawa za kulevya.

### 3.3.2 Kaguzi zilizofanyika katika Kudhibiti Dawa Tiba zenye asili ya Kulevya

Katika kudhibiti dawa tiba zenye asili ya kulevya kaguzi mbalimbali zimekuwa zikifanyika kwenye maduka ya dawa za binadamu na wanyama. Kwa mwaka 2021 kaguzi zilifanyika katika maeneo 30 ambayo yanahusisha maduka ya dawa za binadamu. Aidha, ufuatiliaji wa uingizwaji haramu wa dawa hizi ulifanyika katika vituo vya forodha katika mipaka 12 na katika maeneo ya viwanja vya ndege. Mikoa iliyohusika katika kaguzi hizo ni Mtwara, Dar es salaam, Mwanza, Mara, Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga, Geita, Tanga, Morogoro, Songwe, Rukwa, Katavi na Tabora.

Katika kaguzi hizo, ilibainika kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa kumbukumbu za manunuzi na mauzo ya dawa pamoja na kutumika kwa vyeti vya kughushi kujipatia dawa hizo katika baadhi ya maduka ya dawa yaliyokaguliwa. Hali hii inaacha mianya ya uchepushwaji na kutumika kama mbadala wa dawa za kulevya.

Aidha, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) zilishiriki katika operesheni maalum ya Kimataifa, iliyojulikana kama ‘’GAPZ’’ kwa kila Nchi katika eneo lake. Operesheni hiyo iliratibiwa na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ya Umoja wa Mataifa (INCB) kwa lengo la kufuatilia usafirishaji haramu wa dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Gabapentin, Pregabalin, Xylazine na Zopiclone. Operesheni hiyo ilifanyika katika mashirika yanayojihusisha na usafirishaji wa vifurushi pamoja na vituo vyote vya forodha kwenye viwanja vya ndege, Bandari na mipaka ya nchi kavu. Hata hivyo, Operesheni hiyo haikubaini uingizwaji haramu wa dawa hizo.

**3.3.3 Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika Udhibiti wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya (Public Private Partnership – PPP).**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, kwa kushirikiana na GCLA, TMDA, TRA, MSD na Baraza la Famasi imeendelea kutekeleza mradi wa kushirikisha sekta binafsi kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

Mwaka 2021, Mamlaka kwa kushirikiana na taasisi hizo ilitia 25aish Mkataba wa Makubaliano (Memorandum of Understanding) kati ya Serikali na kampuni **27** zinazojihusisha na kemikali bashirifu na vyama viwili vya umoja wa wadau wa dawa za binadamu ili kuanzisha rasmi kwa ushirikiano huo. Ushirikiano huu umepanua wigo wa udhibiti na kuimarisha matumizi salama ya kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

Kupitia utekelezaji wa mradi huu, Tanzania imeendelea kutambuliwa na Bodi ya Kimataifa ya kudhibiti Dawa za Kulevya (INCB) kuwa ni nchi ya mfano ukanda wa Afrika Mashariki wa UNODC katika kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya na hivyo kupewa jukumu la kuzisaidia nchi **tisa** (9) za ukanda huu kuanzisha ushirikiano huo katika nchi zao. Nchi hizo ni Burundi, Comoro, Eritrea, Ethiopia, Madagascar, Malawi, Mauritius, Rwanda na Zambia.

## 3.4 MABORESHO YA SHERIA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2015

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanahitaji sheria madhuubuti ili iweze kutoa matokeo bora kwa kuwabana na kuwawajibisha wale wote wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya. Kwa kuhakikisha hilo linafanikiwa, sheria imekuwa ikiboreshwa mara kwa mara ili kudhibiti kikamilifu tatizo la dawa za kulevya kwa kuifanyia marekebisho kila inapohitajika.

Marekebisho ya Sheria yaliyopendekezwa yalipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Septemba, 2021 kupitia Sheria ya Marekebisho Madogo, Namba 5 ya Mwaka 2021 (The Written Laws Miscellaneous Amendments Act, No. 5 of 2021). Marekebisho ya vifungu vya Sheria vilivyopitishwa na Bunge ni vifungu cha 2, 4, 14, 15, 15A na 17.

Katika kuongeza ufanisi wa kazi, taasisi zilizokuwa zinahitaji kibali kutoka Mamlaka ili kutekeleza majukumu yao, zimepewa uwezo wa kutekeleza majukumu hayo bila kuomba kibali badala yake watoe taarifa ya utekelezaji.

Pia katika kupunguza mlundikano wa mashauri Mahakama Kuu, sheria imeongeza uzito wa dawa za kulevya za mashambani (bangi na mirungi) kutoka zaidi ya kilo **50** kuwa zaidi ya kilo **100** zinazostahili kufikishwa Mahakama Kuu na kutumikia kifungo cha maisha jela pale mtuhumiwa atakapotiwa hatiani.

Vilevile sheria imeongeza kifungo kisichopungua miaka **30** jela kwa mtuhumiwa wa dawa za kulevya aina ya bangi na mirungi kwa uzito usiozidi kilo **50** za awali na kuwa uzito usiozidi kilo **100**.

Sheria imetamka wazi kwamba mtu akipatikana na kiwango kidogo cha dawa za kulevya kwa matumizi binafsi **ametenda kosa la jinai** tofauti na awali kwa lengo la kukomesha matumizi ya dawa za kulevya.

## 3.5 UTEKETEZAJI WA DAWA ZA KULEVYA

Dawa za kulevya zilizokamatwa huteketezwa kwa mujibu wa sheria ili zisirudi kwenye matumizi na biashara haramu. Uteketezaji huo hufanyika chini ya usimamizi wa Hakimu au Jaji na zoezi hilo hushuhudiwa na Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Idara ya Usalama wa Taifa, Mkemia Mkuu wa Serikali, Baraza la Usimamizi wa Mazingira na waalikwa wengine ambao Kamishna Jenerali ataona inafaa kuwaalika.

Mwaka 2021, uteketezaji wa dawa za kulevya ulihusisha dawa aina ya methamfetamini kilo **355** katika Kiwanda cha Saruji cha Dangote mkoani Mtwara. Hali kadhalika, mashamba ya bangi **110** yenye ukubwa wa hekari **185** ziliteketezwa katika operesheni zilizofanyika nchini kwa ushirikiano kati ya Mamlaka na Jeshi la Polisi. Pia, mashamba ya mirungi hekari **10.5** operesheni iliyofanyika wilayani Same mkoani Kilimanjaro.



*Kamishna Jenerali, Gerald Kusaya akishiriki zoezi la uteketezaji wa ekari kumi za shamba la mirungi, wilayani Same mkoa wa Kilimanjaro.*

### 3.6 KESI ZA DAWA ZA KULEVYA

Juhudi za udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya katika mwaka 2021 zilifanikisha kufunguliwa jumla ya kesi **9,538** katika Mahakama mbalimbali Nchini. Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilisimamia mashauri makubwa **16.** Kati ya hayo Mashauri nane **(8)** yaliamuliwa ambapo mashauri manne

**(4)** Serikali ilishinda na katika mashauri manne **(4)** watuhumiwa waliachiwa huru. Mashauri manne **(4)** yalikuwa katika hatua ya usikilizwaji, matatu **(3)** katika hatua ya kutajwa na moja **(1)** lilikuwa katika hatua ya kusomewa hukumu. Hata hivyo inaendelea kufatilia mwenendo wa mashauri ya yaliyofunguliwa katika Mahakama mbalimbali Nchini.

Idadi ya kesi zilizoripotiwa kulingana na makundi na aina ya dawa za kulevya zimeainishwa katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali Na. 8: Kesi zilizofikishwa Mahakamani mwaka 2021**

| Kundi la dawa | Aina ya Dawa | Kesi zilizoripotiwa |
|---|---|---|
| Dawa za kulevya za viwandani | Heroin | 467 |
| | Cocaine | 81 |
| | Methamphetamine | 02 |
| | Morphine | 01 |
| | **Jumla** | **551** |
| Dawa za kulevya za mashambani | Bangi | 7,679 |
| | Mirungi | 1,308 |
| | **Jumla** | **8,987** |

Katika kuboresha upatikanaji wa haki jinai katika mashauri ya dawa za kulevya Mamlaka imeshiriki vikao kazi vya Jukwaa la Wadau wa Haki Jinai Kitaifa. Lengo la vikao hivi ni kuharakisha mchakato wa upatikanaji haki kwa wakati kwa watuhumiwa wa dawa za kulevya na makosa mengine ya jinai.

# SURA YA NNE

# KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA

## 4.1 UTANGULIZI

Jukumu la msingi katika mkakati wa kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya ni kutoa elimu kwa ili kuiepusha kuingia kwenye matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Sura hii inaelezea hali ya matumizi ya dwa za kulevya nchini, sababu zinazochangia watu kujiiingiza kwenye matumizi yake, madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya pamoja na jitihada zilizofanyika katika kutekeleza mkakati huu.

## 4.2 MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

Dawa za kulevya za aina mbalimbali zimeendelea kutumika nchini kwa makundi mbalimbali ya kijamii. Bangi ikiwa ni dawa ya kulevya inayotumiwa zaidi nchini japokuwa hakuna takwimu halisi zinazoonesha kiwango cha matumizi. Heroin ni dawa ya pili kwa kutumika zaidi nchini, mirungi inafuatia kisha cocaine. Aidha, matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na matumizi ya ugoro na viyeyushi kama gundi na petroli yameendelea kuwepo Nchini katika miaka ya karibuni.

Tatizo la dawa za kulevya nchini, limeonekana kuwa kubwa katika maeneo ya ukanda wa Pwani na miji mikubwa kama vile Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Tanga, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mbeya. Hali hii inadhihirishwa na watumiaji wanaojitokeza kutafuta tiba katika vitengo vya afya ya akili katika hospitali za wilaya, mkoa na rufaa, nyumba za upataji nafuu (sober houses), vituo vinavyotoa tiba saidizi kwa waraibu wa heroin kwa kutumia dawa – MAT na asasi za kiraia. Ingawa hakuna takwimu halisi ya watumiaji wa dawa za kulevya nchini waraibu wapatao 905,902 walijitokeza kupata tiba ya uraibu wa dawa mbalimbali za kulevya nchini katika mwaka 2021.

### 4.2.1 SABABU ZINAZOCHANGIA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

Tanzania kama ilivyo katika maeneo mengine Duniani, matumizi ya dawa za kulevya yameendelea kuleta changamoto katika jamii pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kukabiliana na changamoto hizo. Sababu mbalimbali zinazochangia watu kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya ni kama ifuatavyo: -

a) Kurithi vinasaba vya uraibu, familia ambazo zimeathirika na uraibu na kuwa na vinasaba hivyo husababisha wanafamilia kuingia katika matumizi ya dawa za kulevya. Wazazi wenye uraibu wa dawa za kulevya wana uwezekano mkubwa wa kupata mtoto wenye tatizo hilo.
b) Kushindwa kujitambua (stadi za maisha) miongoni mwa vijana. Hali hii huwasababishia kujiingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya kwa sababu ya kukosa uwezo wa kutambua changamoto zao na njia sahihi za kutatua changamoto hizo.
c) Urahisi na upatikanaji wa dawa za kulevya katika mazingira yetu kama vile bangi na mirungi imekuwa moja ya sababu kubwa ya watu kushawishika kuingia kwenye matumizi ya dawa hizo.
d) Msukumo rika na kufuata mikumbo, ambapo baadhi ya vijana hurubuniwa na kushawishiwa na wenzao wanaotumia dawa hizo. Tatizo hili huwapata mara nyingi vijana wenye malezi duni, wenye mazingira magumu na hatarishi ya kuishi kama vile migodini na watoto wa mitaani.
e) Kutokuwa na uelewa sahihi juu ya madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya kiafya, kijamii na kiuchumi. Asilimia kubwa ya watu wanajiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya kwa lengo la kupata starehe, furaha, kuwa karibu na marafiki au kupunguza makali ya maisha bila kufahamu madhara wanayoweza kuyapata.
f) Migogoro na utengano wa kifamilia imekuwa ikisababisha kukosekana kwa malezi bora kwa watoto na vijana hali inayosababisha kukosekana kwa uangalizi wa karibu na hivyo baadhi yao kujiunga na makundi yanayotumia dawa za kulevya.
g) Watu wenye magonjwa ya akili kama vile saikosisi (kuchanganyikiwa), msongo wa mawazo, sonona na kihoro wamekuwa wakitumia dawa za kulevya kama njia ya kustahimili magonjwa hayo.
h) Ukuaji wa teknolojia, utandawazi na mitandao ya kijamii vimechangia sana kwenye mmomonyoko wa maadili kwa vijana kwa kuiga maisha, mitindo, mila na desturi za kigeni ikiwemo kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya.
i) Kuishi na ndugu, rafiki, mpenzi au mwenza ambaye anajihusisha na dawa za kulevya huchangia katika kuanza matumizi hayo.
j) Matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya bila kufuata ushauri wa daktari. Mfano, mgonjwa akitumia dawa tiba zenye asili ya kulevya kutuliza maumivu anapoamua kutumia kinyume na utaratibu wa tiba alioandikiwa na Daktari, humsababishia kuwa mraibu wa dawa hizo.

k) Imani potofu, mila na desturi za baadhi ya jamii zimekuwa zikichangia matumizi ya dawa za kulevya nchini. Mfano, watu huamini wakitumia bangi hupata nguvu za kufanyakazi zaidi au kusoma zaidi.

## 4.3 MADHARA YA DAWA ZA KULEVYA

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya husababisha madhara ya kiafya, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira kama ilivyoainishwa.

### 4.3.1 Kiafya

Matumizi ya dawa za kulevya husababisha magonjwa mbalimbali yakiwemo ya akili, uraibu, moyo, ini na mapafu. Matumizi ya dawa hizo kwa njia ya kujidunga huchangia kuenea kwa maambukizi ya VVU, virusi vya homa ya ini na kifua kikuu miongoni mwa watumiaji na jamii kwa ujumla. Aidha, matumizi hayo yanaweza kufanya mishipa ya damu kusinyaa na inapotokea hali hiyo kwenye ubongo husababisha shinikizo la damu na kiharusi. Pia, dawa za kulevya hupunguza kumbukumbu, uwezo wa kufikiri na kufanya maamuzi sahihi. Mtumiaji hupatwa na arosto anapokosa kutumia dawa za kulevya. Matumizi ya kiwango kikubwa cha dawa za kulevya kuliko alichozoea mtumiaji, husababisha vifo vya ghafla hasa kwa wajidunga.

Wanawake wajawazito wanaotumia dawa za kulevya huweza kupata changamoto mbalimbali kama kuharibika kwa utaratibu wa mtiriko wa hedhi, kuharibika kwa mimba, kuzaa watoto wenye uraibu wa dawa za kulevya, watoto waliodumaa kimwili na kiakili, kujifungua watoto walio na changamoto nyingi za kiafya kama matatizo ya moyo na ulemavu wa viungo au kujifungua watoto njiti.

Madhara mengine ya kiafya ni pamoja na saratani, upungufu wa nguvu za kiume, sonona, kukosa usingizi, kukosa hamu ya kula na kuoza meno. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya husababisha ulemavu, upungufu wa kinga ya mwili dhidi ya maradhi, vidonda kwenye mfumo wa chakula kama vile vidonda vya tumbo na mara nyingine vifo. Kwa ujumla matumizi ya dawa hizi hupunguza umri wa kuishi wa mtumiaji kutokana na maradhi, uhalifu au kuzidisha kiasi cha dawa.

### 4.3.2 Kijamii

Jamii iliyotulia ni muhimu katika juhudi za kujiletea maendeleo hatahivyo Matumizi ya dawa za kulevya yanapojitokeza katika jamii husika huondoa utulivu na kusababisha; kukithiri kwa vitendo vya kihalifu katika jamii kama vile wizi, ukahaba, utapeli na uporaji. Vitendo hivi hufanyika ili watumiaji wa dawa za kulevya waweze kupata fedha za kununulia dawa hizo. Wafanyabiashara wa dawa

za kulevya huendesha magenge ya utekaji, mapigano na mauaji ili kulinda biashara yao na kuifanya jamii kuishi kwa woga. Wauzaji wa dawa za kulevya wana kawaida ya kujihusisha na biashara nyingine haramu kama vile usafirishaji haramu wa binadamu, kuwaweka watu rehani (bondi), silaha za magendo, uhalifu wa kimtandao, ujangili na madanguro. Pia, huweza kuvuruga usalama kwa kufadhili vita na ugaidi.

Kwa upande wa familia mahusiano huvurugika na watoto kukosa malezi bora na kukimbilia mitaani hali inayosababisha kukosa haki zao za msingi ikiwemo elimu. Dawa za kulevya huongeza kasi ya maambukizi ya VVU, homa ya ini na kifua kikuu katika jamii kutoka kwa watumiaji ambao huwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya maradhi hayo. Unyanyapaa kwa watumiaji husababisha wakose haki zao za kifamilia na kijamii na hata pale wanapoacha matumizi ya dawa za kulevya familia zao au waajiri hushindwa kuwakubali. Pia, matumizi ya dawa za kulevya husababisha ajali zinazoweza kuepukika ambazo husababisha ulemavu, vifo, uharibifu wa mali na miundombinu.

### 4.3.3 Kiuchumi

Matumizi ya dawa za kulevya hupunguza ufanisi kazini na kuweza kusababisha kupoteza ajira au kufilisika. Mtumiaji ambaye hajapata ajira hushindwa kuajirika hivyo kusababisha umaskini kwake, jamii yake na Taifa kwa ujumla. Aidha, watumiaji wa dawa za kulevya hawawezi kujishughulisha na shughuli yeyote ile ya uzalishaji mali hivyo matumizi ya dawa hizo hupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Wafanyabiashara wa dawa za kulevya husababisha mfumuko wa bei na kuondoa mizania ya ushindani wa kibiashara kwa kuwa wana uwezo wa kununua bidhaa kwa bei ya juu kuliko bei ya kawaida ya soko. Hivyo, huwakosesha wengine fursa na kuongeza pengo la kipato kati yao na wananchi wa kawaida, hali inayosababisha umaskini.

Biashara ya dawa za kulevya huambatana na utakatishaji wa fedha haramu zinazotokana na biashara hiyo ambapo madhara yake ni pamoja na kuhamisha nguvu ya kifedha kutoka kwenye Serikali, masoko na wananchi na kwenda kwa wahalifu ambao ni wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Vilevile, utakatishaji fedha huathiri taasisi za kifedha kama vile benki pale mhalifu anapoamua kutoa fedha zake kwa mkupuo ambapo mara nyingi huwa ni kiasi kikubwa na hivyo kuiacha taasisi ya kifedha ikiyumba na kuzorotesha ukuaji wa uchumi.

Jamii na Serikali huingia gharama zisizo za lazima kwa ajili ya udhibiti wa dawa za kulevya ikiwemo ukamataji, matibabu ya waraibu, kutoa elimu ya kupunguza

matumizi ya dawa za kulevya na kutunza wafungwa magerezani badala ya kuelekeza rasilimali hizo kwenye maendeleo. Hali hiyo, hurudisha nyuma jitihada za kukuza uchumi wa nchi.

#### 4.3.4 Kisiasa

Kutokana na uwezo mkubwa wa kifedha walionao wafanyabiashara wa dawa za kulevya, huweza kuingia kwenye siasa ili kukuza biashara ya dawa za kulevya. Pia, wafanyabiashara hao wanaweza kufadhili chaguzi au kuwaondoa viongozi waliochaguliwa kidemokrasia na kuwaweka watu wao madarakani ili kulinda biashara na maslahi yao. Hali hii inaweza kuathiri mustakabali wa nchi kwa kutawaliwa na magenge ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

#### 4.3.5 Kimazingira

Kilimo cha bangi na mirungi mara nyingi hufanyika katika maeneo yasiyofikika kirahisi kama vile kwenye milima, misitu na kwenye vyanzo vya maji na hivyo kusababisha kukauka kwa vyanzo vya maji, ukame, mmomonyoko wa ardhi, kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai na uoto wa asili. Uharibifu huu umejidhihirisha katika baadhi ya safu za milima ya Uluguru, Usambara, Udzungwa, Upare na maeneo ya Arumeru. Aidha, wajidunga wa dawa za kulevya wamekuwa wakisababisha uchafuzi wa mazingira kwa kutupa hovyo vifaa vya kujidungia (sindano) kwenye vichochoro, viwanja vya michezo, fukwe na vituo vya daladala na kuiweka jamii kwenye hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa. Wavutaji wa dawa za kulevya huchafua hewa kwa moshi unaotoka kwenye dawa hizo na kudhuru afya za watu walio karibu nao.

### 4.4 Jitihada zilizofanyika katika kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya

Elimu huleta uelewa kwenye jamii na kuiwezesha jamii husika kujitambua na hivyo kujiepusha na uhalifu wa aina mbalimbali. Kwa kuzingatia umuhimu wa elimu hiyo katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya Mamlaka huratibu na kutoa elimu kwa wadau na maeneo mbalimbali kwa kushirikisha watumishi wa Mamlaka au kukasimisha jukumu hilo kwa asasi za kiraia na wadau wengine.

#### 4.4.1 Uelimishaji ulioshirikisha Mamlaka

i. **Taasisi za elimu**: Mamlaka iliwajengea uwezo walimu **66** wa shule za msingi na sekondari kwenye mikoa ya Mtwara na Mwanza juu ya tatizo la dawa za kulevya ili waweze kupeleka elimu hiyo kwa wanafunzi katika maeneo yao. Mamlaka pia ilitoa elimu kwa wanachuo **400** wa Chuo cha Maendeleo ya

Wananchi Same, wanachuo wapya **500** wa mwaka wa kwanza katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Dar es salaam na wanachuo **200** kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma.

ii. **Mitaala ya elimu**: Mamlaka ikishirikiana na wataalam kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ilifanya mapitio, uchambuzi na uboreshaji wa maudhui ya dawa za kulevya kwenye mitaala ya elimu ngazi ya shule za msingi na sekondari ili kuhakikisha suala la dawa za kulevya linatolewa kwa usahihi kwenye ngazi hizo za elimu.

iii. **Vyombo vya habari:** Mamlaka ilifanya uelimishaji kwa Umma kupitia njia ya redio, runinga, magazeti, majarida, vipeperushi, mitandao ya kijamii, tovuti ya Mamlaka, sanaa na wasanii. Aidha, elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa kwa wahariri wa vyombo vya habari **50**, waandishi wa habari **100** na waandishi wa vyombo vya habari za kidijitali **30**.

iv. **Vyombo vya Ulinzi na Usalama:** Katika kuimarisha ushirikiano katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Mamlaka ilitoa elimu kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya na tiba ya uraibu. Elimu hii ilitolewa kwa Kamati za Ulinzi na Usalama, wadau wa afya, viongozi wa dini, viongozi wa kijamii na asasi za kiraia katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Mwanza na Arusha.

v. **Waendesha mashtaka na wapelelezi**: Elimu kuhusu Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2015 ilitolewa kwa waendesha mashtaka **45** na wapelelezi **44** kutoka mikoa ya Tanga, Kagera na Morogoro. Mafunzo hayo yalihusu namna ya kushughulikia makosa na mashauri ya dawa za kulevya kwa mujibu wa sheria na kanuni zake kama kufanya upelelezi na kufuata taratibu wakati wa upekuzi na ukamataji.

vi. **Wadau wa mapambano ya dawa za kulevya:** Mafunzo ya udhibiti wa dawa za kulevya yalitolewa kwa watumishi **250** wa Shirika la Posta na **175** wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) Nchini. Aidha, elimu ya udhibiti wa uchepushaji wa kemikali bashirifu ulifanyika kwa wadau wa kemikali wapatao **1,922**. Uelimishaji huu umefanyika kwa ushirikiano mkubwa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Waliopatiwa mafunzo hayo ni pamoja na waingizaji wa kemikali, watumiaji wa kemikali, maofisa wa vituo vya forodha vya mipakani, wajasiriamali, wasimamizi wa shughuli za kemikali na madereva wanaosafirisha kemikali hizo. Vile vile, Mamlaka ilifanya uhamasishaji kwa asasi mbalimbali katika mikoa **tisa** (9) ya Tanzania Bara ili elimu ya dawa za kulevya iweze kuifikia jamii kwa karibu zaidi katika maeneo yao. Mikoa hiyo ni Arusha, Moshi, Mtwara, Lindi, Shinyanga, Tabora, Ruvuma, Geita na Simiyu.

vii. **Matukio ya kitaifa**: Elimu ilitolewa juu ya tatizo la dawa za kulevya kwenye Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Dawa za Kulevya Duniani yaliyoadhimishwa kitaifa Jijini Dodoma, Maonesho ya Kimataifa ya Biashara

(Sabasaba) Jijini Dar es Salaam, Maadhimisho ya Wiki ya Vijana, Kumbukizi ya Kifo cha Baba wa Taifa na Kilele cha Mbio za Mwenge mkoani Geita na Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani yaliyofanyika Jijini Mbeya.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa na viongozi alioambatana nao walipotembelea banda la Uelimishaji la Mamlaka kwenye Kilele cha Mbio Maalum za Mwenge wa Uhuru na Kumbukizi ya Siku ya Kifo cha Baba wa Taifa Mwl. Nyerere Wilayani Chato mkoa wa Geita.*

### 4.4.2 Uelimishaji uliofanywa na Asasi za Kiraia na wadau wengine

Katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya nchini, asasi za kiraia chini ya uratibu wa Mamlaka zimeendelea kutoa elimu juu ya tatizo la matumizi na biashara ya dawa za kulevya kwenye shule za msingi, sekondari na vyuo. Elimu hii iliambatana na uanzishwaji na usimamizi wa klabu za kupinga dawa za kulevya mashuleni. Wanafunzi **8,990** wa shule ya msingi na **2,140** wa sekondari walipatiwa elimu hiyo katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021. Aidha, elimu ilitolewa kwa watu wapatao **15,763** kutoka katika makundi mbalimbali ya kijamii.

Asasi za kiraia zilizotoa elimu katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam na Mwanza ni kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 9: Asasi zilizotoa Elimu ya Dawa za Kulevya mwaka 2021**

| Na. | Jina la Asasi |
|---|---|
| 1. | Anti-Alcoholism Drug Addiction |
| 2. | Blue Cross Society Tanzania |
| 3. | Drug Abuse and Prevention Organization (DAPO) |
| 4. | Drug Abuse Fighting and Counselling Organization (DAFCO) |
| 5. | Gift of Hope Foundation |
| 6. | Guluka Kwalala Youth Environment Group |
| 7. | Harakati Network Organization |
| 8. | International Organization of Good Templars (T- IOGT) |
| 9. | Kibao Salama Foundation |
| 10. | Kibwena Community Development |
| 11. | Kimara Peer Educators and Health Promoters Trust Fund |
| 12. | Kirumba Movement for Harm Reduction |
| 13. | Life and Hope Rehabilitation Organization |
| 14. | Matumaini Group |
| 15. | Next Generation Keepers |
| 16. | Ngao Youth Group |
| 17. | Rafiki wa Watoto (RAWATO) |
| 18. | Saikolojia - Sensitization Networking of Tanzania (Saiko Senta) |
| 19. | Women and Child Vision (WOCHIVI) |
| 20. | Youth Achievement Village in Tanzania (YAVT) |
| 21. | Youth and Community Rehabilitation (YCR) |
| 22. | Youth Counseling and Rehabilitation Centre (YCRC) |
| 23. | Youth Empowerment and Psychotherapy Aid Organization (YEPAO) |

### 4.4.3 Uwezeshaji uliofanyika kwenye Asasi za Kiraia na wadau wengine

Mamlaka imeendelea kushirikiana na kuziwezesha asasi zinazojihusisha katika utoaji wa elimu ya dawa za kulevya hapa nchini, kwa mwaka 2021, Mamlaka iliziwezesha asasi 3 zote zikiwa za mkoa wa Tanga ikiwa ni kodi ya kwa nyumba mbili na kujenga sehemu ya kulia chakula kwenye nyumba moja ya upataji nafuu, jumla ya sh 6,300,000/-zilitolewa kwenye asasi hizo, katika kufanikisha hayo Mamlaka pia iliziwezesha asasi zipatazo 9 kupitia fedha kutoka kwenye mfuko wa dunia unaowezesha miradi mbalimbali hapa nchini (Global Fund) jumla ya sh **917,459,182.48** zilitolewa kwa asasi zinazofanya kazi ya kuwaandaa waraibu ili waweze kupata huduma ya methadone. Asasi za kiraia zilipewa fedha kutoka mfuko

wa dunia unaowezesha miradi mbalimbali hapa nchini (Global Fund) ni kama zifuatavyo:-

**Jedwali Na. 10: Asasi zilizowezeshwa na Mamlaka mwaka 2021**

| Na. | Jina la Asasi |
|---|---|
| 1. | Youth and Community Rehabilitationa (YCR) |
| 2. | Gift of Hope Foundation |
| 3. | Organization of Youth Against Risk Behaviour (OYARB) |
| 4. | Youth Volunteers Against Risk Beahaviour (YOVARIBE) |
| 5. | Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA) |
| 6. | Kibao Salama Foundation (KISAFO) |
| 7. | Mapambano ya Kifua Kikuu na UKIMWI Temeke (MUKIKUTE) |
| 8. | Peer to Peer Supporting Group |
| 9. | Steps Tanzania |

# SURA YA TANO

# KUPUNGUZA MADHARA YANAYOSABABISHWA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA

## 5.1 UTANGULIZI

Upunguzaji wa madhara yanayosababishwa na matumizi na biashara ya dawa za kulevya ni nguzo ya tatu kati ya nguzo kuu nne za kudhibiti na kupambana na tatizo hilo. Hivyo, kupitia nguzo hii waraibu wa dawa za kulevya wanapata fursa ya kupata tiba na matatizo mengine ya kiafya, sambamba na kuwapatia stadi za kazi na hatimaye kuwaunganisha na jamii Pamoja na familia zao. Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa tiba, huduma za utengemao pamoja na elimu ya upunguzaji madhara yanayosababishwa na matumizi ya dwa hizo. Huduma hizo zinatolewa kwenye vituo vinavyotoa tiba saidizi kwa waraibu wa heroin kwa kutumia dawa (MAT Clinics), Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) na Vitengo vya Afya ya Akili katika hospitali za wilaya, mkoa na rufaa.

## 5.2 Huduma ya Tiba Saidizi kwa Waraibu kwa Kutumia Dawa (MAT)

Waraibu wa dawa za kulevya aina ya heroin hupewa huduma ya tiba ya dawa ya Methadone na huduma za unasihi (MAT) katika kuwasaidia kuondokana na matumizi ya dawa hiyo. Tangu kuanza kwake mwaka 2011, huduma hii imeendelea kupanuka na kuimarishwa katika maeneo mbalimbali nchini, lengo kuu likiwa ni kuboresha afya ya waraibu.

Pamoja na dawa ya Methadone inayotumika ikiwa katika hali ya kimiminika, Serikali imeingiza dawa nyingine aina ya Buprenorphine iliyo katika hali ya kidonge itakayotumika pia katika matibabu ya waraibu wa heroin. Dawa hii ya Buprenorphine kwa sasa iko katika hatua ya majaribio katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Huduma ya tiba ya uraibu hutolewa sambamba na tiba za magonjwa yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile magonjwa ya akili, UKIMWI, kifua kikuu, magonjwa ya ngono, homa ya ini, saratani na magonjwa mengine. Vilevile, vituo hivi hutoa huduma za tiba kwa watoto waliozaliwa na tatizo la uraibu kutoka kwa mama zao.

Waraibu wa dawa za kulevya huibuliwa na kuandaliwa katika ngazi ya jamii kwa kuwapatia huduma ya unasihi kabla ya kufikishwa katika vituo vya tiba. Kazi ya kuwaandaa waraibu hufanywa na asasi za kiraia zenye uzoefu na tatizo hilo ambazo huwapa elimu ya madhara ya dawa za kulevya, namna bora ya kuachana nazo na huduma za tiba zinazopatikana katika vituo vya MAT na kuwapeleka katika vituo husika kwa hatua ya usajili na kuanza huduma ya tiba.

Hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 huduma za MAT zilikuwa zikipatikana kwenye vituo **11** na vituo vidogo (Satellite) **vinne** na kufanya idadi ya vituo vinavyotoa huduma hiyo kufikia **15** hapa nchini. Vituo hivyo vipo; Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za rufaa za mikoa za Temeke na Mwanayamala na vituo vidogo vinne Segerea, Mbagala Round Table, Vijibweni Kigamboni na Tegeta za mkoani Dar es salaam, Hospitali ya rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya, Hospitali ya rufaa ya mkoa ya Sekou Toure-Mwanza, kituo cha Itega jijini Dodoma, Hospitali ya wilaya ya Bagamoyo na hospitali ya rufaa ya mkoa Tumbi za mkoani Pwani, Hospitali ya rufaa ya mkoa ya Bombo mkoani Tanga, Hospitali ya rufaa ya mkoa Mount Meru - Arusha na Kituo cha afya Tunduma mkoani Songwe.

Jumla ya waraibu **5,759** walipatiwa huduma ya tiba ya Methadone na tiba nyinginezo kulingana na uhitaji katika kipindi cha mwaka 2021. Hata hivyo, Serikali inaendelea kujenga vituo vingine zaidi vya kutolea huduma ya MAT nchini kulingana na uhitaji na uwezo.

**Jedwali Na. 11: Idadi ya Waraibu waliopewa Rufaa kutoka Asasi za Kiraia kwenda Vituo vya MAT, Januari hadi Desemba, 2021**

| Na. | Asasi | Mkoa | Wajidunga | | Watumiaji wa njia zingine | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | Me | Ke | |
| 1. | MEFADA | Dar es salaam | 23 | 1 | 118 | 5 | 147 |
| 2. | MEFADA | Dodoma | 3 | - | 35 | - | 38 |
| 3. | YCR | Dodoma | - | - | 18 | - | 18 |
| | | Bagamoyo | - | - | 129 | 3 | 132 |
| | | Arusha | 19 | 3 | 112 | 8 | 142 |
| | | Dar es salaam | 4 | - | 114 | 1 | 119 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 4. | YOVARIBE | Dar es Salaam | 56 | 2 | 174 | 2 | 234 |
| | | Dodoma | 13 | 2 | 106 | 3 | 124 |
| | | Mwanza | 44 | 1 | 152 | 7 | 204 |
| | | Tanga | 5 | - | 62 | - | 67 |
| | | Arusha | 5 | - | 86 | 5 | 96 |
| 5. | MUKIKUTE | Dar es salaam | 36 | - | 82 | 2 | 120 |
| 6. | KISAFO | Chalinze - Pwani | 1 | - | 4 | - | 5 |
| 7. | OYARB | Kibaha -Pwani | 20 | 1 | 369 | 4 | 394 |
| 8. | Gift of Hope Foundation | Tanga | 18 | - | 103 | 3 | 124 |
| 9. | SETA | Mbeya | 8 | - | 79 | - | 87 |
| 10. | IRDO | Tunduma -Songwe | 4 | - | 87 | 1 | 92 |
| **Jumla kuu** | | | **259** | **10** | **1,830** | **44** | **2,143** |

**Jedwali Na12: Waraibu waliopata Huduma ya MAT mwaka 2011 hadi Desemba, 2021**

| | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|
| **Waraibu waliosajiliwa toka kuanzishwa kwa huduma** | 11,088 | 587 | **11,675** |
| **Waraibu waliokuwa wanatumia Methadone 2021** | 5,485 | 274 | **5,759** |
| **Waliokutwa na maambukizi ya VVU** | 753 | 214 | **967** |
| **Waliokutwa na ugonjwa wa kifua kikuu** | 183 | 9 | **192** |
| **Waliokutwa na maambukizi ya homa ya ini aina B (HBV)** | 191 | 22 | **213** |
| **Waliokutwa na maambukizi ya homa ya ini aina C (HCV)** | 318 | 91 | **409** |

Kulingana na takwimu zinavyoonesha kwenye jedwali hapo juu, magonjwa ambukizi kama vile kifua kikuu, VVU, maambukizi ya homa ya ini aina B na C yameendelea kuwa juu kwa waraibu wa dawa za kulevya ikilinganishwa na maambukizi kwenye jamii. Kati ya waraibu **11,675** waliokuwa wamesajiliwa kupata huduma ya tiba kwenye vituo vya MAT hadi kufikia Desemba, 2021, waliokutwa na maambukizi ya VVU ni **967** ambayo ni asilimia **8.3** ikilinganishwa na asilimia **4.5** kwenye jamii. Maambukizi ya VVU kwa upande wa wanawake waliokuwa wanahudumiwa kwenye vituo hivyo yalikuwa ni asilimia **36.5** ikilinganishwa na wanaume asilimia **6.8.** Hali hiyo inaonesha kuwa wanawake wanaotumia dawa za kulevya huwa kwenye hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU ikilinganishwa na watumiaji wenzao wa jinsi ya kiume.

Maambukizi ya kifua kikuu katika kipindi cha mwaka 2021 kwa waraibu waliokuwa wanapata huduma ni **192** sawa na asilimia **3.33** ukilinganisha na asilimia **0.13** katika jamii (ambao ni watu **133** kati ya watu **100,000)**. Walioambukizwa homa ya ini aina B kwa waraibu walikuwa **213,** sawa na asilimia **3.7** na homa aina C ni **409** sawa na asilimia **7.1** ambapo kwenye jamii maambukizi hayo ni chini ya asilimia **2**. Takwimu hizi za kwenye jamii zinatoka Wizara ya Afya.

### 5.3 Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)

Nyumba za upataji nafuu, ni nyumba ambazo waraibu wa dawa za kulevya hutunzwa na kupatiwa huduma kwa kupitia hatua 12 za upataji nafuu na huduma za unasihi bila kutumia dawa. Serikali imeendelea kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa nyumba hizi ambazo huendeshwa na Asasi za Kiraia au watu binafsi kwa kufuata Mwongozo wa Serikali wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu Tanzania Bara.

Mwaka 2021 huduma hii iliendelea kutolewa katika mikoa mbalimbali kwenye nyumba **44** ikilinganishwa na nyumba **33** zilizotoa huduma hiyo mwaka 2020 ikiwa ni ongezeko la nyumba **11 .** Waraibu wapatao **3,109** walipata huduma hizo, ikijumuisha wanaume **2,949** na wanawake **160** kwa mwaka 2021. Idadi ya waraibu waliohudumiwa kwenye nyumba za upataji nafuu imeainishwa katika jedwali lifuatalo;-

**Jedwali Na. 13: Waraibu waliopata Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu kwa Mwaka 2021**

| Na. | Jina la Nyumba | Mkoa | Waraibu waliopata Huduma | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | Jumla |
| 1. | Arusha Recovery Sober House | Arusha | 105 | - | 105 |
| 2. | Changamoto ni Matumaini | Arusha | 37 | - | 37 |
| 3. | Foundation for Wellness and Youth Tutelage (Olmotonyi Recovery House) | Arusha | 89 | 21 | 110 |
| 4. | Northern Hill Sober House | Arusha | 69 | - | 69 |
| 5. | Tanzania New Future Rehabilitation Organisation | Arusha | 49 | - | 49 |
| 6. | Tanzania Sobriety Change Foundation (Arusha Recovery Sober House) | Arusha | 150 | - | 150 |
| 7. | Tanzania Sobriety Change Foundation (Meru Recovery Sober House) | Arusha | 120 | - | 120 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. | Tanzania Sobriety Change Foundation (Njiro Recovery Sober House) | Arusha | 125 | - | 125 |
| 9. | Tanzania Sobriety Initiative | Arusha | 56 | - | 56 |
| 10. | Tanzania Sobriety and Rehabilitation Organization | Arusha | 45 | - | 45 |
| 11. | Arise and Shine Sober House | Dar es Salaam | 21 | - | 21 |
| 12. | Changamoto ni Matumaini | Dar es Salaam | 72 | - | 72 |
| 13. | Drug Abuse Prevention Organization | Dar es Salaam | 16 | - | 16 |
| 14. | Drug Free Tanzania – The Right Way Recovery House | Dar es Salaam | 54 | - | 54 |
| 15. | Drug Free Tanzania – The Ties That Bind Us Recovery Center | Dar es Salaam | 47 | - | 47 |
| 16. | Hope Again Rehabilitation and Wellness Foundation | Dar es Salaam | 15 | 3 | 18 |
| 17. | Kipepeo Foundation – South Beach Sober House | Dar es Salaam | 40 | | 40 |
| 18. | Morogoro Recovery Center 1 | Dar es Salaam | 52 | - | 52 |
| 19. | Morogoro Recovery Center 2 | Dar es Salaam | 51 | - | 51 |
| 20. | Morogoro Recovery Center 3 | Dar es Salaam | 78 | - | 78 |
| 21. | Morogoro Recovery Center 4 | Dar es Salaam | 124 | - | 124 |
| 22. | Morogoro Recovery Center 5 | Dar es Salaam | 71 | - | 71 |
| 23. | Morogoro Recovery Center (Women House) 6 | Dar es Salaam | - | 18 | 18 |
| 24. | People with Drug Dependence and Relief Foundation | Dar es Salaam | 56 | 17 | 73 |
| 25. | Pillimissanah Foundation | Dar es Salaam | 148 | 27 | 175 |
| 26. | The Awaited Rehabilitation Center | Dar es Salaam | 22 | - | 22 |
| 27. | Tanzania Sobriety and Rehabilitation Organization | Dodoma | 28 | - | 28 |
| 28. | Iringa Sober House | Iringa | 52 | - | 52 |
| 29. | Sobriety Forever Rehabilitation Center | Kagera | 16 | - | 16 |
| 30. | Kilimanjaro Community Recovery Organization | Kilimanjaro | 111 | - | 111 |
| 31. | Kilimanjaro New Vision and Sobriety | Kilimanjaro | 98 | 25 | 123 |
| 32. | Kilimanjaro Recovery Center | Kilimanjaro | 107 | 6 | 113 |
| 33. | Kilimanjaro Recovery Home | Kilimanjaro | 36 | - | 36 |
| 34. | Kilimanjaro Sober House | Kilimanjaro | 18 | - | 18 |
| 35. | Kipepeo Foundation – Free at Last Sober House | Morogoro | 31 | - | 31 |
| 36. | Pillimissanah Foundation | Mwanza | 89 | - | 89 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 37. | Life and Hope Rehabilitation Organization | Pwani | 241 | - | 241 |
| 38. | Mamaz and Papaz Sober house | Pwani | 21 | - | 21 |
| 39. | New Vision of Life Society Sober House (Second Chance for Addicts) | Pwani | 116 | - | 116 |
| 40. | Tabora Sober House | Tabora | 79 | - | 79 |
| 41. | The Light of Miracle Organization - Women's Hope Rehabilitation | Pwani | - | 43 | 43 |
| 42. | Courage on Recovery Foundation | Tanga | 80 | - | 80 |
| 43. | Gift of Hope Foundation | Tanga | 58 | - | 58 |
| 44. | Tanga Drug Free Organization | Tanga | 56 | - | 56 |
| | **Jumla** | | **2,949** | **160** | **3,109** |




*Watumishi wa Mamlaka pamoja na Afisa Maendeleo ya Jamii (Jiji Arusha) wakiwa katika picha ya pamoja na waraibu wanaopata nafuu walipotembelea moja ya Nyumba za Upataji Nafuu, Jijini Arusha.*

## 5.4 Tiba ya Uraibu wa Dawa za Kulevya katika Vitengo vya Afya ya Akili Nchini

Serikali imeendelea kusimamia na kuimarisha jitihada za uboreshaji wa utoaji huduma ya tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya katika vitengo vya afya ya akili vilivyopo katika hospitali mbalimbali Nchini. Jumla ya waraibu **891,117**, ambapo wanaume **454,390** na wanawake **436,727** walipatiwa huduma ya tiba ya uraibu katika vitengo vya afya ya akili kwenye hospitali hizo kwa mwaka 2021. Idadi kubwa ya waraibu walionekana kuathirika zaidi na matumizi ya vilevi kama vile pombe, bangi, tumbaku (sigara), mirungi, heroin na cocaine. Aidha, kutokana na kuadimika pamoja na kupanda kwa gharama za unuuzi wa dawa za kulevya kulikotokana na kuimarika kwa udhibiti wake, baadhi ya waraibu hao waligundulika kutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya zinazotumika hospitali kama vile valium, pethidine na tramadol, eneo ambalo linahitaji kuongezewa nguvu za udhibiti.

**Jedwali Na14: Idadi ya Waraibu Waliopata Tiba kwenye Vitengo vya Afya ya Akili Nchini kwa mwaka 2021**

| Na. | Hospitali ya Mkoa | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mwananyamala (DSM) | 45,678 | 51,348 | 97,026 |
| 2 | Temeke (DSM) | 33,479 | 46,987 | 80,466 |
| 3 | Bombo | 23,467 | 16,543 | 40,010 |
| 4 | Mount Meru | 18,970 | 11,340 | 30,310 |
| 5 | Amana (DSM) | 24,589 | 33,876 | 58,465 |
| 6 | Morogoro | 18,009 | 12,034 | 30,043 |
| 7 | Mawenzi | 9,875 | 13,568 | 23,443 |
| 8 | Maweni | 11,230 | 16,543 | 27,773 |
| 9 | Musoma | 17,854 | 7,896 | 25,750 |
| 10 | Sekou Toure | 27,654 | 19,876 | 47,530 |
| 11 | Bukoba | 29,801 | 13,456 | 43,257 |
| 12 | Shinyanga | 13,467 | 14,564 | 28,031 |
| 13 | Geita | 11,765 | 9,234 | 20,999 |
| 14 | Manyara | 8,790 | 10,987 | 19,777 |
| 15 | Tumbi | 25,601 | 32,034 | 57,635 |
| 16 | Dodoma | 17,865 | 9,876 | 27,741 |
| 17 | Singida | 8,765 | 4,356 | 13,121 |
| 18 | Tabora | 7,654 | 5,673 | 13,327 |
| 19 | Katavi | 9,803 | 8,976 | 18,779 |
| 20 | Rukwa | 5,674 | 8,970 | 14,644 |
| 21 | Njombe | 7,862 | 7,843 | 15,705 |
| 22 | Iringa | 13,421 | 12,398 | 25,819 |
| 23 | Mbeya | 18,973 | 16,789 | 35,762 |
| 24 | Ruvuma | 8,976 | 9,087 | 18,063 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 25 | Simiyu | 9,786 | 11,203 | 20,989 |
| 26 | Mtwara | 9,875 | 13,543 | 23,418 |
| 27 | Lindi | 6,543 | 7,864 | 14,407 |
| 28 | Songwe | 8,964 | 9,863 | 18,827 |
| | **Jumla** | **454,390** | **436,727** | **891,117** |

### 5.5 Faida ya Huduma za Upunguzaji Madhara kwa Waraibu

Utoaji wa huduma za upunguzaji madhara kwa waraibu wa dawa za kulevya umeonesha manufaa ya moja kwa moja kwa waraibu na jamii ambapo waraibu wanapata fursa ya tiba ya uraibu wa dawa za kulevya. Yafuatayo ni manufaa yanayotokana na huduma hizo;-

i. Kupunguza uraibu na madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya;
ii. Kupata huduma za tiba kwa magonjwa mengine yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya kama vile UKIMWI, homa ya ini, kifua kikuu na magonjwa ya ngono;
iii. Kupunguza uwezekano wa kupata usugu wa dawa za kufubaza makali ya UKIMWI na vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu;
iv. Kupungua kwa vifo vya ghafla vinavyotokana na kuzidisha kiasi cha matumizi ya dawa za kulevya;
v. Kupunguza unyanyapaa na kukubalika katika jamii;
vi. Kuondoa mifarakano katika familia na kupunguza watoto wa mitaani;
vii. Kurudisha ufahamu na utimamu wa mwili kwa waraibu wa dawa za kulevya na kuweza kujishughulisha na shughuli za uzalishaji mali na kuondoa utegemezi;
viii. Kupungua kwa vitendo vya uhalifu katika jamii;
ix. Kupungua kwa rushwa na mzunguko wa fedha haramu kwenye jamii; na
x. Kupungua kwa biashara ya dawa za kulevya.

# SURA YA SITA

# USHIRIKIANO WA KIMATAIFA, KIKANDA NA KITAIFA KATIKA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA TANZANIA

## 6.1 UTANGULIZI

Dawa za kulevya ni tatizo la kidunia ambalo huendeshwa na mitandao ya kihalifu iliyopo maeneo mbalimbali duniani. Mkakati huu umeainisha jinsi serikali ilivyoshirikiana na wadau mbalimbali kitaifa, kikanda na kimataifa katika kukabiliana na tatizo hilo. Hata hivyo, ushirikishwaji uliofanyika katika taasisi za ndani ya nchi zimeainishwa katika sura ya tatu, nne na tano, hivyo sura hii itazungumzia ushirikiano wa kikanda na kimataifa. Mwaka 2021 katika kutekeleza mkakati huu Mamlaka ilifanikiwa kushiriki katika maeneo yafuatayo: -

## 6.2 USHIRIKIANO WA KIKANDA

Serikali ya Tanzania imekuwa ikipambana na tatizo la dawa za kulevya katika ngazi ya kanda kwa kushirikiana kwa karibu na Umoja wa Afrika (AU) wenye makao makuu jijini Addis Ababa, Ethiopia. Umoja huo umekuwa ukitoa miongozo ya kisera na kimkakati katika kupambana na tatizo hilo. Vilevile, nchi yetu imeendelea kushiriki mikutano inayojumuisha nchi za Msumbiji na Afrika Kusini katika kufuatilia wafanyabiashara wakubwa wa dawa za kulevya kwa kubadilishana taarifa za kiintelijensia zinazohusu dawa za kulevya, uhalifu wa kupanga na kufanya operesheni za pamoja *Trilateral Planning Cell (TPC)*. Vilevile, nchi yetu imeendelea kushiriki katika Mkutano wa kila mwaka wa Viongozi wa Vyombo vinavyopambana na dawa za kulevya Afrika ujulikanao kama HONLEA Afrika. Lengo la mkutano huo wa kila mwaka ni kubadilishana uzoefu, kushirikiana katika upatikanaji wa taarifa pamoja na kupanga mikakati ya pamoja katika udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya barani Afrika.

Vilevile, taasisi za nje za CDC, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (GF) na EU-ACT zimekuwa mstari wa mbele katika kutoa mafunzo ya upunguzaji uhitaji wa dawa za kulevya pamoja na tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya. Aidha, taasisi hizi kwa kushirikiana na Mamlaka zimeweza kuratibu mafunzo kwa watoa huduma wa afya kuhusu uraibu na tiba ya methadone kwa waathirika wa dawa za kulevya nchini.

## 6.3 USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

Tanzania imeendelea kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC) kwa kutekeleza mikataba yote ya kimataifa inayohusiana na udhibiti wa dawa za kulevya, kemikali bashirifu ya mwaka 1961, 1971 na 1988 pamoja na mikataba mingine ya kikanda. Mwaka 2021, Mamlaka ilishiriki Mkutano wa 64 wa Kamisheni ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya jijini Vienna, Austria ulioratibiwa na UNODC chini ya Tume ya Kimataifa ya Kudhibit Dawa za Kulevya (CND). Aidha, kwa kushirikiana na Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (INCB), Mamlaka imeweza kuanzisha ushirikishwaji wa sekta binafsi kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Vilevile, Mamlaka imeshiriki katika mikutano, semina na warsha mbalimbali zinazolenga mikakati maalum ya udhibiti wa biashara ya dawa za kulevya na kemikali bashirifu zilizoratibiwa na INCB kwa njia ya mtandao.

Aidha, Mamlaka ilishiriki katika maandalizi ya Mradi wa kuisaidia Serikali ya Tanzania katika kudhibiti uhalifu mkubwa wa kupangwa (Serious Organized Crimes-SOC) ulioitishwa na Wizara ya Katiba na Sheria ikifadhiliwa na UNDP kwa ushirikiano na Serikali ya Uingereza na Kamisheni ya Umoja wa Ulaya.

Mamlaka ilihudhuria mafunzo juu ya upekuzi na ukamataji wa dawa za kulevya kwenye vyombo vya majini yaliyoandaliwa na UNODC nchini Msumbiji na katika visiwa vya Shelisheli. Pia, Mamlaka ilishiriki semina zilizoratibiwa na INCB kwa njia ya mtandao kuhusu; biashara ya dawa za kulevya na utakatishaji fedha; ufuatiliaji wa uteketelezaji wa mradi wa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu; mashauriano ya pamoja kimataifa juu ya hatua za kuchukua katika kudhibiti ongezeko la kemikali zisizodhibitiwa ili zisitumike kwenye uzalishaji wa dawa za kulevya pamoja na jitihada za ushirikishwaji wa sekta ya viwanda katika kudhibiti kemikali bashirifu.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania zilishiriki katika operesheni maalum ya Kimataifa iliyojulikana kama ‘’GAPZ’’. Operesheni hiyo iliratibiwa na INCB kwa lengo la kufuatilia usafirishaji haramu wa dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Gabapentin, Pregabalin, Xylazine na Zopiclone katika mashirika yanayojihusisha na usafirishaji wa vifurushi pamoja na vituo vya forodha vya mipakani.

### 6.4 Ushirikiano na Taasisi nyingine za Kimataifa

Serikali imekuwa ikishirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa katika kupambana na kudhibiti tatizo la dawa za kulevya katika maeneo makubwa matatu ya kimkakati ambayo ni ukamataji, utoaji wa elimu, kinga na tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya. Baadhi ya wadau wakubwa katika mashirikiano hayo katika upande wa ukamataji wa wauzaji na wasambazaji wa dawa za kulevya ni pamoja na Drug Enforcement Adminstration (DEA) ya Marekani na National Crime Agency (NCA) ya Uingereza. Kutokana na ushirikano huo, Mamlaka ilifanikiwa kupata mafunzo na taarifa zilizosaidia kukamata dawa za kulevya ambazo zilipitia baharini.

Vilevile, taasisi za nje za CDC, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (GF) na EU-ACT zimekuwa mstari wa mbele katika kutoa mafunzo ya upunguzaji uhitaji wa dawa za kulevya pamoja na tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya. Aidha, taasisi hizi kwa kushirikiana na Mamlaka zimeweza kuratibu mafunzo kwa watoa huduma za afya kwa waraibu wa dawa za kulevya.

# SURA YA SABA

## CHANGAMOTO NA HATUA ZA BAADAYE

### 7.1 UTANGULIZI

Katika utekelezaji wa mikakakti ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya nchini, Mamlaka ilipata mafanikio mengi kama ilivyoainishwa kwenye sura mbalimbali za taaraifa hii na pia ilikumbana na changamoto kadhaa. Changamoto na mikakati iliyowekwa ili kukabiliana nazo imeainishwa kama ifuatavyo;-

### 7.2 CHANGAMOTO

i. Upungufu wa vitendea kazi na vifaa vya kiufundi kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa za wafanyabiashara wa dawa za kulevya, utambuzi wa dawa za kulevya na operesheni za ukamataji.
ii. Kubadilika mara kwa mara kwa mbinu za kusafirisha na usambazaji wa dawa za kulevya
iii. Kuibuka kwa dawa mpya za kulevya zinazotengenezwa na kemikali bashirifu zinazohitaji teknolojia ya kisasa kuweza kuzitambua.
iv. Uhaba wa wataalam wa masuala udhibiti wa dawa za kulevya mipakani, viwanja vya ndege, vituo vya kutolea tiba ya uraibu na kwenye kampuni za usafirishaji.
v. Ukosefu wa maabara mahsusi kwa ajili ya utambuzi wa haraka wa dawa za kulevya
vi. Mahitaji makubwa ya huduma za utengamao kwa waraibu wanaopata nafuu hususan mafunzo ya ujasiriamali, mitaji na vifaa.
vii. Uwezo mdogo wa Serikali katika kusaidia sekta binafsi zenye asasi za kudhibiti tatizo la matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo Nyumba za Upataji Nafuu

### 7.3 MIKAKATI

i. Kutoa na kushiriki mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi wanaohusika na udhibiti wa dawa za kulevya ili waweze kupata maarifa mapya yatakayoendana na mabadiliko ya mbinu za wafanyabiashara wa dawa za kulevya.
ii. Kufanya ufuatiliaji wa maabara bubu zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya kama methamphetamine ambayo ni rahisi na nafuu kuitengeneza kuliko heroin.

iii. Kuanzisha maabara ya sayansi jinai kwa ajili ya uchunguzi na utafiti wa dawa za kulevya, kemikali bashirifu, dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na dawa mpya za kulevya (NPS).

iv. Kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya zinazozalishwa Nchini kwa kufanya operesheni za uteketezaji wa dawa za kulevya za mashambani mara kwa mara katika mikoa inayolima bangi na mirungi kwa wingi ikiwemo Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Pwani

v. Kuitangaza namba 119 ambayo ni ya bure kwa ajili ya kupokelea taarifa juu ya masuala mbalimbali yanayohusu dawa za kulevya na watu wanaojihusisha na biashara hiyo haramu.

vi. Kuimarisha ushirikianao na wadau wa ndani na nje ya nchi ili kuongeza ufanisi katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya.

vii. Kuongeza idadi ya vituo vya kutolea tiba ya uraibu wa dawa za kulevya

viii. Kuhamasisha sekta binafsi kuchangia rasilimali za aina mbalimbali katika udhibiti wa tatizo la matumizi ya dawa za kulevya

ix. Kuongeza ushirikiano na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka katika kuendesha mashauri ya dawa za kulevya Mahakamani

# NOTES

NOTES